

MKUU KULIKO

SULEMANI YUPO HAPA

 “Naamini.” Hebu tuendeleo kusimama sasa kwa dakika chache, tunapoinamisha vichwa vyetu. Sijui, tunapoviinamisha vichwa vyetu, na mioyo yetu, kwamba kama kuna haja maalum usiku wa leo ambayo ungehitaji kwa Mungu, kitu maalum, ungeifanya ijulikane kwa mkono wako ulioinuliwa. Yeye anajua kile tu unachohitaji sasa. Ndani ya moyo wako, wazia tu kile ilicho.

² Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha sana usiku wa leo kwamba tuna majaliwa hayo makuu ya kusema “Baba” kwa Muumba wa mbingu na nchi. Pia tuna furaha sana kujua ya kwamba tumekusanyika hapa usiku wa leo katika mahali pa Mbinguni katika Kristo, Mwana Wako. Naye aliahidi ya kwamba kama tungeomba chochote katika Jina Lake tungepewa. Bwana, Wewe—Wewe umeona kila mkono ulioinuliwa. Wewe—Wewe unajua kilichokuwa nyuma ya mkono huo. Kulikuwako na haja kwa ajili ya kitu fulani, nami ninatoa maombi yangu pamoja na yao. Kwa imani sasa tunakuja kwenye Kiti kikuu cha Enzi cha pembe za ndovu cha Mungu. Hapo, tunapoiona Damu ya Bwana Yesu imewekwa pale juu ya madhabahu, kuhakikisha ya kwamba ombi letu limejibiwa. Jambo moja tu limesalia: kama tutaamini kwamba tutapokea yale tuombayo, basi tutapewa. Saidia kutokuamini kwetu.

³ Pia, Baba, tunaomba usiku wa leo ya kwamba tunapolifungua Neno, kwamba Wewe utatufunulia Hilo. Wewe Ndiwe uliyeliandika Hilo, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utalifanya Hilo lijulike kwetu. Kisha uje miongoni mwetu na kuliishi Hilo na kujithibitisha Mwenyewe, kwamba katika saa hii ya ufanisi mkuu wa kisayansi, na wakati kanisa linakuwa baridi na kupotoka kuingia katika utaratibu na kanuni za imani, kwamba Wewe unabaki yule yule kwa wale wanaokuamini Wewe kuwa yule yule, kwamba Wewe ni Mungu yule yule uliyezimwaga nguvu kwenye Pentekoste. Wewe ni Mungu yeye yule aliyetembea na wale wanafunzi, Yule aliyekuwa pamoja na Musa nyikani, na Wewe ni yeye yule usiku wa leo. Tubariki pamoja sasa tunaposhiriki kwenye Neno. Katika Jina la Yesu Kristo tunaomba. Amina.

Ketini.

⁴ Kama kawaida, nayahesabu kuwa ni majaliwa makuu kuwa ambapo watu wa Mungu wemekusanyika pamoja, kwa kuwa nina hakika ya kwamba Kristo yuko miongoni mwetu. Nasi

tunamshukuru Bwana Mungu kwa kusikia taarifa nzuri ya jana jioni, na ingali inaonyesha ya kwamba Mungu huwaponya wagonjwa na wanaoteseka. Na sasa kuna... Laiti tungaliweza tu kuweka nia zetu zimetulia juu ya Kristo, na kujua Uwepo Wake upo hapa, na kwamba tayari amewanunulia kila baraka ya ukombozi aliyofia Yeye. Ni zenu. Yote mnayopaswa kufanya ni kuamini hilo.

⁵ Na sasa tunatumaini ya kwamba mlikuwa na pumziko zuri leo. Nanyi... Nitajaribu kuwaachilia mtoke usiku wa leo, upesi tu iwezekanavyo. Halafu basi kesho usiku, ikiwa ni Alhamisi usiku; na kisha Ijumaa usiku; na halafu Jumamosi asubuhi, kile kiamshakinywa.

⁶ Ninataka kuliomba kusanyiko usiku wa leo haja kutoka kwa Ndugu Carl Williams, kwenye tawi la Phoenix, rais wa tawi la Phoenix. Baba yake mwenye umri wa miaka themanini na mitano alishikwa na kiharusi alasiri ya leo. Naye alikuwa awe hapa usiku wa leo. Na ilimbidi kuruka kwa ndege kaskazini mahali fulani, kumwona baba yake. Ndipo nikaingia kwa maombi kwa ajili ya jamaa huyo mkongwe mara moja. Majuma machache yaliyopita nilikuwa pamoja naye, alikuwa mchangamfu kuliko mwanawe, huko Albuquerque ambako tulikuwa na mkutano. Na usiku wa leo yuko kitandani, kiharusi, umri wa miaka themanini na mitano. Lakini ninaamini kwa moyo wangu wote kwamba Mungu atamwondolea kiharusi hicho. Ni—ni—ninaamini hilo, mnaona, kwa kuwa nilipokuwa katika maombi ni—ningeweza kumwona tu akisogea. Na yeye—yeye... Huna kiharusi, wakati unapoweza kusogea, mwajua. Kwa hiyo, yeye, ni—ninajua atapata nafuu, kama si kupata afya.

⁷ Nasi tunashukuru kwa ajili ya i—imani, ushahidi, kitu fulani pamoja nasi kinachotwambia, nasi tunajua. Hakuna kubahatisha tena ndani yake. Tumekuwa, kwa miaka, na Neno la Mungu. Sasa tunaye Mungu wa Neno, mnaona, na papa hapa akiliishi Neno Lake. Kwa hiyo ni kweli, moja ya ishara kuu za mwisho zilizoahidiwa Kanisa kabla ya Kuja kwa Bwana.

⁸ Sio muda mrefu uliopita, mimi na mwanangu tulikuwa... tulienda Bombay, India, ambako nafikiri tulikuwa na wito mkubwa zaidi wa madhabahuni niliopata kuona Bwana akifanya katika mikutano yetu. Ulikuwa... Tusingeweza kukadiria ni wangapi waliomjia Kristo, kwa sababu ilikadiriwa yapata nusu milioni katika kusanyiko moja, yapata laki tano. Na kulikuwa na wakati mgumu sana ukiendelea. Na kulikuwako na Mabanyani, wale watu watakatifu. Na, loo, jamani, nena kuhusu dini, India inayo! Alasiri hiyo, nilikaribishwa na dini kumi na saba mbalimbali za India, na kila moja yao ilimkana Yesu Kristo: kila moja yao: Islamu, Budha, Kalasinga, Jaini, loo, wengi sana wao. Nami sikusema kitu. Niliwasikiliza tu. Vile, ilitubidi kuvua viatu vyetu, kuingia kwenye hekalu la Jaini.

⁹ Usiku huo, mbele ya halaiki ambayo singeweza kuona mwisho wao, na wakati watu walipoanza kuja; ilibidi jeshi la mgambo kuwaruhusu watu kuja, mmoja mmoja. Wa kwanza kuja, alikuwa ni mwenye ukoma; hakuwa na mikono, na masikio yalikuwa yameliwa. Mtu yeyote alijua tatizo lake lilikuwa ni nini, bila shaka. Na kisha baada ya wawili ama watatu kupita pale, mbona, huyo hapo Roho Mtakatifu, akifunua. Hakika, upako unaposhuka, basi unaweza kujua yale watu wanawazia. Mnaona, unalipata. Nao walikuwa wakiwazia ilikuwa ni kitu kama kuwasiliana kimawazo.

¹⁰ Na mtu yeyote, anayejua telepathia ni nini, angeninii, ingekuwa ni... Kama ulifikiri ya kwamba kitu kama Roho Mtakatifu kutambua ingekuwa ni telepathia, mbona, basi, hujui mengi juu ya telepathia.

¹¹ Kwa hiyo basi hawa watu watakatifu, na Maraja, na kadhalika, kwenye mito yao na... Kwa hiyo walikuwa wamelundikana mmoja juu ya mwingine, ambapo wawili au watatu walikabwa roho mpaka wakafa, mkutanoni, na wakijaribu tu kulundikana ndani. Nami nilikuwa tu na siku mbili za kukaa.

¹² Na nisingeweza kupata ulinzi... Sababu, ilibidi niupate mjini, ilikuwa ndiyo njia pekee tungepata ulinzi. Nje ya mji, kulikuwako na mama aliyepitia kule, ambaye alikuwa amesababisha ghasia kidogo, na wawili au watatu wakachomwa visu wakafa, nao wasingenipa ulinzi nje ya mji. Na bila shaka lilikuwa ni jambo la kuchukiza sana kuona.

¹³ Lakini yapata mtu wa nne kuja, alikuwa ni wa nne ama wa tano, alikuwa ni mtu kipofu, naye alikuwa ni ombaomba. Bila shaka, India ina watu milioni mia nne na sabini, na ilionekana kwangu kama milioni mia nne wa hao walikuwa ni ombaomba. Sijawahi kuona ombaomba wengi hivyo! Na ni jambo la kuhuzunisha sana. Wakati, hatujui jinsi tulivyo matajiri, mpaka ikubidi kufanya ziara kama hiyo, mara moja.

¹⁴ Huyu hapa mama amelala barabarani, maskini mtoto wake anakufa kwa njaa. Ufizi wake umeshikamana na midomo yake. Maskini ninii yake... Hawezi kulia tena. Mamaye yuafa kwa njaa, pia. Anataka kukupa mtoto huyo mchanga, asije akafa; chochote kile, asije akafa. Na hapa, vema, utamchukua? Huyu *hapa* mwingine, huyu *hapa* mwingine, mwingine, loo, wewe, kweli hapana mwisho wake. Nao hao hapo, na ni la kusikitisha sana. Nao ni wanadamu ambao Kristo aliwafia.

¹⁵ Na hapo, usiku huo, nikisimama pale, ndipo mtu huyu kipofu akaja. Roho Mtakatifu akasema, sasa, "Yeye ni ombaomba, pia ni mwabudu jua. Amekuwa kipofu miaka ishirini." Vema, mara hayo yaliposemwa, ungeweza kushika, unajua. Wanakufanya wewe...

¹⁶ Unapoenda mahali kama hapo, afadhali ujue unachozungumzia, maana watakupa changamoto kwake, wakati wowote tu. Na ni afadhali uwe na hakika ya kwamba Mungu alikutuma. Huigizi kanisa kule. Inakubidi kweli kuwa na kile unachozungumzia. Ni sawa hapa Marekani, bali kamwe usijaribu kuingia hudumani 'sipokuwa una hakika kabisa. Halafu basi huko Afrika, na hao wachawi na kadhalika, hao ni—hao wanawasiliana na mizimu. Hawajipumbazi tu na saikolojia. Hao ni—hao wamepagawa na pepo, na wana nguvu. Na inahitaji tu nguvu za Mungu, zinaweza kuzishinda. Na sijapata kuona wakati, hata hivyo, ila ule ambao Bwana wetu mkuu na mwenye utukufu Yesu alipita juu ya hayo yote, na kupata ushindi kila wakati. Ninasema hilo kama mtumishi Wake, katika Jina Lake.

¹⁷ Basi usiku huu kule, kulikuwako, ninakumbuka, mtu huyu. Alisema, “Wewe ni kipofu.” Kasema, “Wewe ni ombaomba, pia unaabudu jua.”

¹⁸ Nao wanaamini, wakiangalia jua mpaka wapofuke, kwamba wataenda Mbinguni; kwa hiyo kuna Mbingu kwa ajili yao, nao wataenda, kwa, wanaabudu maumbile.

¹⁹ Basi, sikilizeni, ungeihisi ikija, ya kwamba wao, hao, hasa wale wanaowaita watu watakatifu. Ndipo wanajipaka mafuta ya mizeituni; ni tamasha la kuangalia; wanachinja mbuzi na kuabudu.

²⁰ Kwa hiyo basi, aliyefuata, Huyo alisema, “Wewe ni mtu umeoa, na una watoto wawili. Nao ni wavulana wawili. Na mmoja wao ana umri wa miaka sita hivi, na huyo mwingine tisa hivi.” Ndipo wakati mfasiri alipomwambia hivyo, hiyo ilikuwa sahihi. Na hata hivyo wasingesikiliza hayo. Walidhani ilikuwa ni saikolojia.

²¹ Ndipo nikawaza, “Bwana, laiti ungenionyesha jambo ambalo wangeweza kuona likitendeka.”

²² Nawe huna budi kuangalia yale Roho Mtakatifu anayosema. Hayo ndiyo anayokwambia. Kaa hapo muda mrefu kutosha mpaka usikie anachokujibu. Unaona? Sikiliza anachokwambia. Kwa sababu, si mimi. Sijui lolote kulihusu. Ni Yeye. Na hata sijui ninalosema, mimi mwenyewe, na sijui mpaka nitakapoisikia kanda. Na, basi, kwa hiyo basi ni ajabu kuona kile Yeye alichofanya.

²³ Ndipo basi nikaona, na nikamwona mtu huyo, kama ono, amesimama juu, naye angeweza kuona. Alifunguliwa macho. Nikawaza, “Huu utakuwa ni wakati mzuri sana sasa hivi.”

²⁴ Nami nikasema, “Leo hii nilikaribishwa katika hekalu la Jaini, ambamo wengi wenu viongozi mbalimbali hapa walikuwako. Nanyi mlikuwa mkiniambia jinsi Ukristo ulivyokuwa duni, na jinsi dini yenu ilivyokuwa kubwa. Sikuwa na nafasi ya kumtetea Bwana Yesu. Lakini,” nikasema,

“usiku wa leo, huyu hapa mtu amesimama hapa, aliye kipofu. Sasa kama ningemwuliza kasisi wa Kiislamu, ama kasisi wa Kibudha, ama yeyote yule, ni kitu gani kilichosababisha awe hivyo, mngesema alikosea, kwa sababu aliabudu maumbile badala ya muumba. Ningesema ‘amina’ kwa hilo. Hiyo ni kweli, ‘Maumbile badala ya muumba.’

²⁵ “Vema, sasa, ikiwa mtu huyu ndio kwanza aseme ya kwamba angemtumikia Mungu aliyemrudishia kuona kwake! Sasa ameona kwamba amekosea. Sasa mngemfanyia nini? Ninyi Wabudha mngemfanya aachane na mungu wake aje ajiunge na Ubudha. Waislamu wangemfanya kuwa Mwislamu. Na zingine mbalimbali. Ni kitu gani? Mgebadilisha tu mawazo yake. Mngeninii tu. . . Ni saikolojia.”

²⁶ Nikasema, “Marekani imejaa jambo lilo hilo. Wamethodisti wote wanataka kuwabadilisha Wabaptisti. Nao Wabaptisti wanataka kuwabadilisha Wapentekoste. Nao wa Umoja wanataka kuwabadilisha wa Uwili. Wa Uwili wanataka kubadilisha. . .” Loo, jamani, sijawahi kusikia kitu kama hicho! Ila jambo moja la shukrani, sote tunamwabudu Mungu yule yule. Lakini kule ni tofauti.

²⁷ “Lakini,” nikasema, “ni saikolojia. Hakika kuna Muumba mahali fulani aliyeyaumba macho yake.” Sasa, nisingalisema hivi kama nisingalilionna lile ono kwanza. Maana, hiyo. . .

²⁸ Nina umri wa miaka hamsini na nne, nimeona maono tangu nilipokuwa na umri wa miezi kumi na minane. Si hata wakati mmoja. . . Nitamwuliza mtu yeyote ikiwa wamewahi kuona moja likishindwa. La, bwana. Kamwe halitashindwa. Kamwe halikushindwa na kamwe halitashindwa. Daima ni sahihi, kwa sababu ni Mungu.

²⁹ Halafu basi nilijua mtu huyo alikuwa anaenda kupata kuona kwake, bali nilikuwa nikijaribu kutega mtego mdogo kuwashika baadhi ya hao wasioamini. Pia nikasema, “Sasa, kama dini ya Kiislamu, ambayo ndiyo dini kubwa hapa India, hebu makasisi wa Kiislamu pale, waje hapa na kurejesha kuona kwa mtu huyu, nami nitakuwa Mwislamu.” Mnaona? Nikasema, “Kama Budha ni dini kubwa hivi, acha makasisi wa Kibudha waje, ama yeyote yule.” Nikasema, “Hakika, kama mtu huyu anataka kuwa sawa na Mungu wa kweli, hakika Muumba mkuu Yule aliyeyafanya macho yake mara ya kwanza anaweza kumfanyia macho mara ya pili, kama anataka kuyatumia kwa utukufu Wake.” Hilo lilikuwa ndilo kusanyiko nyamavu kuliko yote niliyowahi kusikia.

³⁰ Nikasema, “Sasa, jukwaa liko wazi, basi hebu mtu anayeweza kuja hapa na kumpa kuona kwake. . . Hebu Mungu, aliye Mungu wa kweli, Yule aliyemwumba kwa kuanzia, aliyeyaumba macho yake, hebu aje na kurejesha kuona kwake, nami niko tayari ku—kuwa mfuasi wa dini hiyo.” Hakuna mtu aliyesema neno.

³¹ Nikasema, “Ninajua yale mnayofikiria. Mnafikiria kwamba ninatumia telepathia kuelewa matatizo ya watu hao, na kadhalika, na kuwaambia kile walicho, wao ni akina nani. Hata siwezi kuyasoma majina yao; inanibidi kutaja tahajia zake. Siwezi kulitamka. Hata siwezi kuzungumza lugha yao. Mnaita hayo saikolojia. Kama ndivyo, sijui jambo moja kuhusu saikolojia. Nanyi ndio mabingwa wake. Hebu bingwa huyo wa saikolojia aje na kumpa mtu huyu kuona kwake basi. Tuone kama saikolojia inaweza kurejesha kuona kwa kipofu.” Hilo lingali lilikuwa kusanyiko nyamavu. Hakuna mtu aliyesema hata neno.

³² Nikasema, “Mbona hamsemi kitu? Hakika kuna Mungu mahali fulani. Yote, yote haya, kila kitu kinachoendelea, kinathibitisha kuna Mungu mahali fulani. Yeye ni nani?” Nikasema, “Sababu ya ninyi kutokusema chochote, ni kwa sababu hamwezi kufanya hivyo. Wala na mimi. Bali Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Mwanawe, Yesu Kristo, Yule niliye shahidi Wake, amenionyesha ono ya kwamba mtu huyu atapata kuona kwake. Sasa, ikiwa Yeye hatafanya hivyo, basi mimi ni nabii wa uongo; nifukuzeni kutoka India. Lakini kama Yeye akifanya hivyo. . . Papa hapa, ninyi watu mlio Waislamu, hawa hapa makasisi wenu wamesimama na majoho yao. Hawa hapa Mabudha, na wengine mbalimbali. Mnawaona viongozi wenu, jinsi walivyo kimya? Hawasemi chochote. Lakini ninazungumza. Niliona ono la mtu huyo, atapata kuona kwake, na ataona sasa. Na asipopata, basi kuna kasoro fulani, mimi ni shahidi wa uongo wa Biblia na wa Kristo.” Kila mtu. . .

³³ Nikasema, “Ni wangapi wenu hapa watakaompokea Yeye kama Mwokozi wenu ikiwa Mungu atarejesha kuona kwa kipofu huyu?”

³⁴ Na kila mahali ungaliweza kuona, mikono myeusi tu imeinuliwa, umbali ungaliweza kuona. Vema, ilikadiriwa, watu laki tano. Hiyo ni nusu milioni. Kwa hiyo hao ni wengi mara nyingi, nyingi zaidi kuliko labda walioko Tucson. Kwa hiyo hao hapo, walikuwa wameketi mahali pamoja.

³⁵ Nikakaribia, nikamwomba mtu huyo anikaribie. Nikamkumbatia kwa mikono yangu. Hawafasiri maombi. Nikasema, “Bwana Mungu, hii ni changamoto kwa imani yangu mwenyewe. Lakini papa hapa, wakati makafiri hawa wote wakiwa wamezunguka hapa, hivi Wewe si ni Mungu yeye yule ambaye ulikuwa daima?” Kisha nikasema, “Sasa ni sifa Zako zilizo hatarini. Mimi ninasema tu yale uliyosema Wewe. Na tangu nikiwa mtoto, Wewe hunionyesha maono, nami sijawahi kuona moja likishindwa. Sasa Wewe ulinionyesha mtu huyu atapata kuona kwake. Ninaitia kuona kwake, katika Jina la Yesu Kristo.”

³⁶ Ndipo mtu huyo akapiga yowe kubwa mno. Naye meya

wa mji alikuwa ameketi pale, akakimbia, akamshika na kumkumbatia. Mtu huyo angeweza kuona vizuri kama ninavyoweza kuona ama mtu mwingine yeyote. Ndipo, nikaona maelfu mara maelfu.

³⁷ Enyi marafiki, sitaki kusema hili kwa kukosoa, bali tumeshindwa kutekeleza mpango ambao Kristo alituma tupate kutekeleza. Mnaona? Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili.” Sasa, hakusema jengeni shule. Hakusema jengeni makanisa. Ambayo, yote ni mazuri. Bali tumeweka wakati wetu wote kujenga shule na makanisa na madhehebu, ambayo yametimiza sehemu fulani. Bali hilo silo alilosema Yeye. “Mkaihubiri Injili, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kwa maneno mengine, kuhubiri Injili kungekuwa ni kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu. Na hapo ndipo tumeshindwa.

³⁸ Kanisa linahitaji, usiku wa leo, sio kitu fulani laini chotara, chororo na dhaifu kama lilivyo kanisa, kufanya tu maungamo, kubatizwa, na wewe ni—wewe ni Mkristo. Kuwa Mkristo ni kujikana. “Jikane mwenyewe. Beba msalaba wako. Unifuate Mimi kila siku.” Siku hizi ni dhaifu sana, nao watu wanajiita Wakristo. Wakati, ilikuwa inamaanisha kifo, kumkiri Kristo, na ilibidi umtegemee Yeye kila siku kwa ajili ya kila kitu ulichohitaji.

³⁹ Mungu yuyo huyo yu hai leo. Ninajua kwamba hiyo ni kweli. Na Yeye ni mkuu tu leo kama alivyokuwa wakati huo. Kama Yeye aliwahi kuwa Mungu, Yeye angali ni Mungu. Lakini ikiwa Yeye si Mungu, basi kamwe hajawahi kuwa Mungu, kwa sababu Yeye ni Mungu wa jamii yote ya binadamu.

⁴⁰ Inafaidi nini kuongea juu ya Mungu wa Ibrahimu, kama Yeye si Mungu yule yule leo hii? Ingefaidi nini kuongea juu ya Mungu Yule aliyeweza kuifungua Bahari ya Shamu, kama Yeye asingeweza . . . kwa ajili ya watoto Wake kuponyoka, kama Yeye asingeweza kufanya jambo lile lile leo hii? Vipi kuhusu Mungu ambaye angeweza kumfufua mtu aliyekufa kutoka kaburini, kama hawezi kufanya jambo lile lile leo hii?

⁴¹ Inafaidi nini kumpa kurumbizi wako punje nzuri na vitamini, kukuza mifupa mizuri yenye nguvu, na mabawa, na manyoya, kisha umweke kwenye kizimba? Atazitumiaje?

Inafaidi nini kufundisha Biblia ya Mungu fulani mkuu?

⁴² Mtu anayeganda anawezaje kupata . . . Anaweza kupata joto kwa moto wa kuchorwa? Mtu anayeganda hata kufa, nawe unamchorea moto, na kusema, “Huo ndio uliokuwako.” Hivyo siyo. Haina budi kuwa ninii . . . Haina budi kuwe na joto kutoka kwake, li—lipate kumsaidia.

⁴³ Na lazima kuwe na uhalisi katika Kuzaliwa upya, kwa kuzaliwa mara ya pili, kujazwa na Roho, na kujua Uwepo wa Mungu upo hapa, na kumwona Yeye akilitekeleza Neno

Lake na ahadi Yake kama tu Yeye alivyofanya. Yesu alisema, “Nikinuliwa juu kutoka duniani, nitawavuta watu wote Kwangu.”

44 Bwana na atusaidie. Sikutaka kuenda kando juu ya hayo, bali ni kuzungumza tu. Bwana awabariki sasa. Basi moja ya siku hizi usiku, labda, kabla haujaisha, nitawahubiria labda usiku mmoja. Nitawahubiria tu.

45 Ninazungumza juu ya uponyaji wa Kiungu sasa kwa sababu ninataka kuona, nikimngojea Bwana labda kufanya jambo fulani. Hilo litaninii . . .

46 Mwajua, yapata asilimia themanini na sita ya huduma ya Yesu ilikuwa ni uponyaji wa Kiungu. Na sisi hatutumii uponyaji wa Kiungu kama jambo kubwa. Huwezi kulifanya kubwa jambo dogo, tunajua hilo, na fani hii kuu ya uponyaji wa Kiungu.

47 Ndio kwanza nimalizie somo, miaka minne au mitano iliyopita, la Kanisa la mwanzoni. Nilianzia na kitabu cha Foxe cha wafia imani, nikashuka nikaja kwa *Babeli Mbili* cha Hislop, na kadhalika, na kote kupitia kwa Nikea, na *Baada ya Nikea* na *Wazee wa Nikea*, na baraza la Nikea, na kuona ya kwamba baada ya kifo cha Yesu Kristo. Kote kupitia Polycarp, na Ireneo na Martin, na wengi wa hao watakatifu mashuhuri, kwa mamia ya miaka baada ya kifo cha Yesu Kristo, waliishindania ile Imani, ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuna kwa lugha, na kuwafufua wafu, na kuwaponya wagonjwa. Ilikuwa ni katika zile nyakati za giza Kitu hiki kilipotelea.

48 Lakini, loo, Mungu alisema, “Nitarejesha,” asema Bwana, “miaka yote iliyoliwa na nzige, na madumadu.” Yeye aliahidi kufanya hivyo, na hii ndiyo saa ya kurejeshwa. Ule Mti utachanua tena. Ninaamini.

49 Bwana awabariki sasa. Na katika Maandiko, ninataka kuchukua somo dogo linalojulikana usiku wa leo, kuwafahamisha tu yale tunayojaribu kufanya. Mnaona, mkiweza . . .

50 Laiti ningelifanya kusanyiko hili liwe katika moyo mmoja, kuona na kujua hasa ya kwamba Yesu Kristo yu hai na yupo hapa miongoni mwenu! Loo, mnaliamini kimawazo ama kiakili. Lakini wakati inapoweza kwenda kupita akili, mpaka unaijua, basi jambo fulani litatukia, mnaona, mnapoweza kutambua. Jambo pekee ni kwamba, ni, kumwona Kristo miongoni mwetu.

51 Mnajua, huko Durban, Afrika Kusini, ambako kulikadiriwa, viti vya magurudumu elfu ishirini na tano, makasha machakavu na mikokoteni, nao wanawakokota watu kutoka misituni, majuma na majuma, wakipitia kule. Kwenye ombi moja, maneno machache tu ya maombi, nao wakasimama na kuondoka hapo. Ndipo kesho yake asubuhi . . .

⁵² Sidney Smith, unaweza kumwandikia telegramu, umwandikie barua. Yeye ndiye meya wa Durban, karibu mara mbili, mara tatu ukubwa wa Tucson. Naam, kubwa mara nyingi kuliko hapo. Nasi tulikuwa kwenye uwanja wa mbio za farasi ambapo alikuwa na watu mia mbili na hamsini elfu wamekusanyika.

⁵³ Ndipo akanipigia simu, kasema, “Ndugu Branham, nenda kwenye dirisha lako linaloangalia pwani.” Hiyo ni Bahari ya Hindi kule. “Utaona kitu hujawahi kuona.”

⁵⁴ Ndipo yakaja yapata kumi ya hayo malori makubwa ya Kiingereza, labda urefu wa futi arobaini, hamsini, yamejazwa tu kabisa mikongojo mikuukuu, na viti vya magurudumu, na vitu walivyokuwa wamechechemea navyo kutoka nyikani, siku moja kabla, nao wakaponywa. Nao hawa hapa, nao wa—watu waliokuwa kwenye viti hivyo na kadhalika, urefu wa jengo la mji, wakifuata nyuma. Wote katika moyo mmoja, wakipita hotelini mwangu wakitembea, wakiimba, “Amini tu. Mambo yote yawezekana,” katika lugha ya uenyeji wao. Ambapo, tulikuwa tumeweka kumbukumbu ya wenyeji elfu thelathini waliompokea Kristo kama Mwokozi wao, kwenye wakati mmoja.

⁵⁵ Sio kuwadharau dada zetu, bali hili hapa jambo ambalo siwezi kuelewa ninapokuja nyumbani. Kila mwaka, ninapoondoka na nirudi, ninakuta wanawake we—wetu wa Marekani wakijivua nguo zaidi, na hata hivyo wakijiita wenyewe Wakristo, wakiimba kwenye kwaya.

⁵⁶ Nao hao wanawake wakisimama pale, wengi wao, bila chochote ila maskini kijitambaa cha 4-H. Na mara wakimpokea Yesu Kristo kama Mwokozi, hakuna mtu aliyepaswa kuwaambia walikuwa uchi. Waliikunja mikono yao, namna *hii*, kuondoka katika uwepo walipokuwa wamesimama wanaume.

⁵⁷ Ikiwa Uwepo wa Yesu Kristo utaleta maarifa hayo kwa mwanamke ambaye hakuwahi kujua lolote kumhusu Yeye, na ndio kwanza ampokee kama Mwokozi, na kumfanya atambue yuko uchi, unapaswa kufanya nini kwa wa—watu hapa wanaodhaniwa kuwa wamestaarabika, na—na wanadhaniwa kuwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kila mwaka wanaendelea kujivua nguo? Kwa ninii... Ninaamini kuna kasoro mahali fulani. Huenda iko na mimi; kama ndivyo ilivyo, kuna kasoro na Neno. Ninaamini ya kwamba Roho Mtakatifu atamfanya mtu avae nguo badala ya kuzivua.

⁵⁸ Sasa fungueni pamoja nami katika Mathayo, mlango wa 12, kifungu cha 38 na hadi kifungu cha 42, Maandiko madogo tu yanayojulikana tunaposoma. Sikilizeni kwa makini sasa.

Hapo baadhi ya waandishi na Mafarisayo wakamjibu, wakasema, Mwalimu, twataka kuona ishara kwako.

Akajibu, akawaambia, Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara, wala hakitapewa . . . ishara yoyote, ila ishara ya nabii Yona.

Kwani kama vile Yona alivyokuwa siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.

Watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Na malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani, na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁵⁹ Kama napaswa kuliita somo, ningetaka kuchukua hayo maneno matano ya mwisho: *Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa.*

⁶⁰ Tunaona, Yesu hapa alikuwa akikaripia. Alikuwa azikemea sehemu zile alizokuwa, na alikuwa amewathibitishia watu ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, kama vile tu Yeye alivyokuwa akituonyesha jana usiku. Na mafundisho yao yote yalikuwa yamekuwa ni kuamini ya kwamba hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi. Na hata kwa maskini mwanamke huyu tuliyenena habari zake jana usiku, yule mwanamke kisimani, jinsi ambavyo yeye, katika hali yake ya uzinzi, na hata hivyo alijua zaidi kuhusu Mungu, na kumtambua Yeye zaidi, kuliko waandishi na Mafarisayo walivyofanya.

⁶¹ Kwa kuwa, walipona hili likitendwa, walilitangaza Hilo kuwa ni namna fulani ya pepo, kasema, “Ni Beelizebuli.” Beelizebuli alikuwa ni mkuu wa pepo, roho, ibilisi. Na kusema kwamba Yeye alikuwa akifanya hayo kwa mizimu fulani, kama mpiga ramli. Na mtu yeyote anajua ya kwamba upiga ramli ni wa ibilisi. Na kwa hiyo walimshtaki Bwana wetu kwa kufanya hivyo.

⁶² Na Yeye akasema, “Kama mkiniita Mimi Beelizebuli, itasamehewa. Lakini mkinena dhidi ya Roho Mtakatifu, wakati Huyu atakapokuja, basi hamna msamaha kwa ajili yake, kwa sababu mnamwita Roho wa Mungu, anayezitenda kazi hizo, ‘roho mchafu.’ Huko ni kumkufuru Roho Mtakatifu.”

⁶³ Mama yangu alizoea kuniambia, nilipokuwa mvulana mdogo, ya kwamba, “Kumkufuru Roho Mtakatifu, kulikuwa, kujiua.” Vema, hivyo sivyo. Mnaona? Biblia inalifundisha, ya kwamba, “Kumkufuru Roho Mtakatifu, ni—ni kuninii, kunena dhidi ya Roho Mtakatifu.” Kukufuru, ni kuzungumza kuhusu. Basi unapomwona Roho Mtakatifu akitenda jambo fulani, nawe

ukamdhihaki Huyo, umevuka mpaka ambao hutaweza kuvuka urudi tena. Kamwe hutasamehewa.

⁶⁴ Kwa hiyo Yesu alikuwa amewaambia, na alikuwa akisema vile Yeye alikuwa—alikuwa akilithibitisha Neno, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Nao iliwapasa kujua hilo, kwa sababu kiongozi wao, Musa, aliwaambia, “Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii mithili yangu.”

⁶⁵ Na sasa walipoona mambo hayo yakitukia, wangali hawakumwamini Yeye. Sio kwa sababu...Ni—ninaamini walimwamini Yeye, bali hawakutaka kukiri hilo, kwa sababu ya mapokeo yao, kwa sababu Mafarisayo walikuwa wamesema, “Mwanamume yeyote au mwanamke ambaye angemkubali Yeye angefukuzwa kwenye sinagogi mara moja.” Nao wanapenda mapokeo yao kuliko walivyolipenda Neno la Mungu lililothibitishwa.

⁶⁶ Na wakati haujabadilisha, sana, hili. Mnajua, Mungu humtwaa mtu Wake bali kamwe si Roho Wake. Shetani humtwaa mtu wake bali kamwe si roho. Huyo hurudi moja kwa moja juu ya mtu mwingine, na kuendelea moja kwa moja huko chini. Na sasa tunalipata katika kila kizazi, karibu ni sawa.

⁶⁷ Naye Yesu alikuwa amejitambulisha Mwenyewe dhahiri. Yeye alisema, “Nisipozitenda kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi. Lakini nikizifanya kazi za Mungu, basi ziaminini hizo kazi.”

⁶⁸ Na ndipo tunaona haya yote, na wangali hawakuamini. Nao wakaja Kwake, wakisha kuyaona mambo hayo yote, na kisha wakasema, “Bwana, sisi tungetaka kuona ishara kutoka Mbinguni.”

⁶⁹ Sasa, tunaona tabaka lile lile la watu linalotaka kusema, “Vema, hakuna kitu kama mwujiza. Hebu nione ukifanywa. Hebu niuangalie kwa macho yangu. Hebu niuchunguze.” Vema, mtu huyo kabisa hana matumaini. Kwa kuwa, kama ukipata kuokolewa, ni mwujiza. Unaweza tu...Huna budi kumwamini Mungu. Huwezi kueleza mwujiza.

⁷⁰ Vipi kama Musa angalisema, “Ninaamini nitachukua baadhi ya majani haya, yanayowaka moto, na kuyapeleka kule kwenye maabara na kuyafanyia uchunguzi, nione ni kitu gani, ni kwa nini hayateketei”? Mungu kamwe asingalizungumza na yeye.

⁷¹ Lakini yeye—yeye—yeye alikuwa...alitambua kwamba ilikuwa ni mwujiza kwamba majani hayo, ule mti, haukuteketea. Kwa hiyo akakaribia apate kuzungumza nao, na kuvua viatu vyake, na kujinyenyekeza mbele zake. Ndipo Mungu akasema naye.

⁷² Sasa, kama tutafanya jambo lile lile, Mungu atasema nasi. Lakini inakubidi kutambua ya kwamba ni Mungu. Na njia pekee

utakayopata chochote kutoka kwa Mungu, ni kumwamini Yeye. “Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini kwamba Yeye yupo.”

⁷³ Sasa, kama tulikuwa tukiona mambo yakifanywa ambayo si ya Kimaandiko, basi ungekuwa na mahali pa kuuliza swali. Lakini wakati imethibitishwa kikamilifu kwa Maandiko, na kisha yakatambulishwa na Mungu Yule aliyeyaandika Maandiko na kutoa ahadi, basi inatupasa kuvua viatu vyetu, tuseme, na kusema, “Bwana Mungu, mimi hapa.” Hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya.

⁷⁴ Na hivyo ndivyo wao, badala ya hilo, walikuja na kusema, “Tunataka kuona mwujiza.” Sasa, kila mtu ni watafuta miujiza.

⁷⁵ Tunaona ya kwamba hata ibilisi, alipomwona Yesu katika hali hiyo ya njaa, alisema, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, yaamuru mawe haya yawe mkate.” Unaona? “Kama wewe,” hakuwa na hakika. Ila alitaka Yeye afanye mwujiza ili aweze kuona. Sasa, hiyo tu ndiyo njia. Unaona?

Unaamini mwujiza. Unaamini, kuona mwujiza.

⁷⁶ Ndipo tunaona, viwanjani, tunapojua ya kwamba Yeye alitambua na angeweza kujua mawazo yao, na kujua ni nani aliyemgusa. Na maisha Yake yote yalikuwa—yalikuwa mfano wa miujiza, na Yeye hakujiipatia sifa kwake. Yeye alisema, “Si mimi nizifanyaye hizo kazi. Ni Baba Yangu. Yeye anaishi ndani Yangu. Yeye huzitenda hizo kazi. Na amin nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe. Ila lile ambalo amwona Baba analitenda, hilo atenda Mwana vile vile.” Mnaona? Yeye alimpa Baba sifa zote. Na Yeye huyo hapa, akienda kote, akitenda kazi hizi.

⁷⁷ Na halafu baada ya hayo yote, walipomkamata pale juu uwanjani, na wakaweka kitambaa usoni Mwake, namna *hii*, na kuchukua fimbo ya hawa askari walevi. Wakasimama pale, wakimpiga kichwani, na halafu wanapeana fimbo, mmoja kwa mwingine, na kusema, “Kama Wewe ni Nabii sasa, tabiri utwambie ni yupi aliyekupiga. Tutakuamini.” Alijua ilikuwa ni yupi.

⁷⁸ Lakini, unaona, mtu wa Mungu, ama mtumishi wa Mungu, hamfanyii ibilisi vitimbi. Unaona? Haiwalazimu kufanya hivyo.

⁷⁹ Mmewasikia wakisema, “Vema, kama kuna kitu kama hicho. . . Nyinyi watu mnaamini uponyaji wa Kiungu. Ninajua ambapo mtu fulani ni mgonjwa. Nenda hapa hospitalini, kundi zima lao.”

⁸⁰ Hiyo labda ingekuwa kama kundi lile lile, hapo kipofu Bartimayo alipojitokeza, wakati walipokuwa wakimdhihaki Yeye, huenda walisema, “Aise, tulisikia Wewe huponya, Wewe huwafufua wafu. Tunayo makaburi yaliyojaa hao hapa juu, watakatifu. Kwea ukawafufue, iwapo Wewe huwafufua wafu.” Mnaona, maskini ibilisi yule yule mkosoaji.

⁸¹ Wakati alipokuwa ananing'inia msalabani, yeye alisema, "Ikiwa Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka hapo na sisi tutakuamini Wewe." Mnaona? Angaliweza kufanya hilo. Walimpa Yeye sifa, na hawakujua walifanya hivyo. Walisema, "Aliwaokoa wengine. Mwenyewe hawezi kujiokoa." La hasha. Kama alijiokoa Mwenyewe, asingeweza kuwaokoa wengine. Kwa hiyo Yeye alijitoa Mwenyewe, kuwaokoa wengine. Nina furaha kwamba Yeye alifanya hivyo. Hakika. Mnaona? Sasa tunamwona kule, mnaona.

⁸² Lakini ni roho yule yule wa kale, "Wewe fanya kitu hapa. Hebu nione kikitendeka." Mbona, Mungu asingeweza kufanya kazi mahali palipokuwapo na kitu kama hicho.

⁸³ Yesu aliingia kwenye umati wa watu wakati mmoja, na kusema msichana aliyekufa alikuwa tu amelala, nao wakamcheka kwa dhihaka. Ndipo Yeye akawatoa nje, kila mmoja, nje ya nyumba, kabla ya Yeye kumfufua. Mnaona? Ilimbidi kufanya hivyo.

⁸⁴ Wakati mmoja alimchukua kipofu, akamwongoza nje ya mji na kumtemea mate machoni mwake, kusudi, apate kumpeleka mbali na umati.

⁸⁵ Palipo na kutokuamini, Mungu hawezi kutenda kazi. Inakupasa kuwa na imani. Basi kama tungeweza kujiweka katika hali hiyo, usiku wa leo, kushuku kila shaka, na kuamini kila Neno la Mungu, na kujua ya kwamba Yesu Kristo yu hai, na ni Yeye anayejionyesha Mwenyewe, basi, nitawaambia, magazeti yataandika vichwa vya habari huku—huku Tucson asubuhi. Ni kitu gani kingetukia humu jengoni, kama mngeingia kwenye moyo huo!

⁸⁶ Lakini watu hawa waliokuwa wameyaona mambo haya yote yakifanywa, na kusikia habari zake, na jambo hilo, na iliwabidi kuyajibu makusanyiko yao. Iliwabidi kusema ilikuwa ni kitu fulani. Yalifanywa. Nao wakasema, "Ni Beelizebuli." Na kwa hiyo wakaja huku, kasema, "Sasa, tunatafuta mwujiza. Tungetaka ishara kutoka Mbinguni, tutataka ishara kutoka Kwako." Alikuwa tayari amefanya ishara nyingi sana, kwa hiyo Yeye kamwe, hakuna Andiko lililosema Yeye alifanya ishara zozote.

⁸⁷ Sasa, Mungu, katika nyakati zote, kamwe hajakuwa bila shahidi. Mungu wakati mwingine ameshuka kwa mtu mmoja pekee. Lakini Yeye daima amekuwa na shahidi, mtu fulani aliyemwamini Yeye, mtu ambaye angeweza kuamini katika mambo ya kimbinguni, mtu ambaye angeweza kumwamini Mungu, jinsi tu ilivyoandikwa na vile tu Yeye alivyo. Ndipo Yeye akawarejelea hapa, kama tunavyoona. Katika nyakati zote, Yeye alikuwa na mashahidi Wake kila mahali.

⁸⁸ Sasa Yeye alirejea hapa, mahali pamoja, kwa "Yonas," anavyoitwa hapa, bali tunamwita Yona. Na watu wengi

humkosoa Yona, na kusema, “Loo, maskini Yona!” Mmelisikia jina hilo. Ila nataka kuninii—ninataka kumtetea Yona, kwa muda kidogo.

⁸⁹ Yona hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Yona alikuwa katika mapenzi ya Bwana. Yeye alikuwa ni nabii. Alirejewa, na kuitwa katika Biblia, “Nabii, Yona.” Naye hakuwa nje ya mapenzi ya Bwana. Nilisoma kidogo, maelezo fulani juu yake, kama historia, wakati fulani uliopita.

⁹⁰ Na sasa, Yona kweli aliambiwa na Bwana ashuke aende Ninawi, mji ulio na ukubwa mara nne ama tano wa mji huu hapa. Nao ulikuwa, kule, mji mkuu wa biashara wa ulimwengu. Ninawi ulikuwa, katika siku hiyo, umerudi nyuma sana. Na—nao walivua samaki baharini. Na walikuwa wameliacha Neno la Mungu la kweli na lililo hai, wakaanza kuabudu wanyama na—na wanyama wakali wa baharini, na kadhalika. Walikuwa katika hali mbaya sana ya mchafuko. Mungu akamwambia, “Shuka uende Ninawi.”

⁹¹ Na sisi tunaona ya kwamba alishuka akaja ufukoni mwa bahari na kuchukua meli kwenda Tarshishi. Sasa, mtu fulani angeamini hapo ya kwamba yeye alifanya kile hasa Mungu alimwambia asifanye.

⁹² Hebu tuone kama hatua za mwenye haki haziongozwi na Bwana. Na kama tunamtumaini Yeye kwa moyo wetu wote, ingawa tunafanya kosa, Mungu atalifanya litende kazi vinginevyo kwa utukufu Wake.

⁹³ Yona! Tunaona, huko nje baharini, kwamba dhoruba zilianza kuvuma, nayo meli ikaanza kuyumbayumba huku na huku, na matumaini yote kwamba wangeweza kuokolewa yaliisha. Naye Yona labda alikuwa akihubiri, siku chache usiku kabla ya hapo, na alikuwa amechoka. Basi alikuwa chini kwenye sakafu ya meli, akijipumzisha kidogo kwa usingizi wa mchana, kwa namna fulani akilala kidogo. Nao wakashuka wakaja na kumwambia, “Amka, Ewe mvivu, ukamwite Mungu wako.”

⁹⁴ Ndipo Yona akasema, “Sasa, nitawaambia yale ninayotaka mfanye. Ninawatakeni muifunge mikono yangu nyuma yangu, na miguu yangu, mkanitupe nje ya meli.” Kisha kasema, “Ndipo meli itaacha kuyumbayumba, mawimbi, meli; yataacha kuiyumbisha meli, kwa maneno mengine, ikiwa tu mtanitupa nje.”

⁹⁵ Kwa hiyo, mnaona, walipofanya hivyo, na kumtupa nje, Mungu alikuwa na samaki mkubwa aliyetayarishwa, ambaye tunaamini kuwa ni nyangumi.

⁹⁶ Na sasa hilo linabishaniwa na sayansi. Hapa, miaka michache iliyopita, nilikuwa huko Louisville, Kentucky, ng’ambo tu ya mji wangu wa nyumbani wa Jeffersonville, Indiana. Ni Mto Ohio tu unaoitenganisha miji hiyo miwili. Nao walikuwa na nyangumi, kiunzi cha mifupa ya nyangumi,

juu ya—juu ya mkokoteni. Basi kulikuwa na mtu aliyesimama pale, ambaye alikuwa akitoa hotuba juu ya nyangumi huyu. Ndipo akasema. . . Sasa, akapanda juu. Nikawaza, “Sijui kama yeye. . . Yeye atasema nini?”

⁹⁷ Alikuwa akizungumza juu ya ukubwa wa kinywa chake, jinsi ambavyo mtu angeweza kutembea aingie kinywani mwake kwa urahisi, kisha kasema, “Mnajua ile hadithi ya Biblia wanayosimulia,” huku akiwa na tabasamu kubwa mno la oposamu kote usoni mwake. Naye akasema, “Mnajua, wao walisema juu ya nyangumi kummeza Yona.” Kasema, “Ninawatakeni mjue kwamba hilo halingewezekana.” Akasema, “Kwa sababu, kama mtaliangalia koo la nyangumi,” kasema, “hata. . . hata lisingepitisha si zaidi ya mpira wa i—inchi nne kupita kwa mharara wake, kupitia kooni mwake.” Kasema, “Hiyo haikuwa hivyo. Hiyo ni hadithi ya uongo tu.”

⁹⁸ Hiyo ilizidi sana kwa hasira yangu ya Kiairishi, kuvumilia hiyo. Nikasema, “Samahani. Ndivyo ilivyo.”

⁹⁹ Akasema, “Bwana,” akasema. “Huyu hapa nyangumi,” akasema, “na ni nyangumi wa aina kubwa.” Akataja ilichokuwa. Kasema, “Enda pale nyuma, kama unataka kujiridhisha, ukalipime koo alilipaswa kupitia, ndipo uniambie ikiwa mtu mzima angeweza kupitia kwenye koo hilo.”

¹⁰⁰ Nikasema, “Ni kwa sababu tu wewe ni asiyeamini.” Nikasema, “Huyu alikuwa ni nyangumi aliyefanywa maalum. Mungu alisema, ‘Alimwandaa samaki.’ Alikuwa maalum, aliyetayarishwa. Angeweza kumwandaa mmoja wa kutupa mkokoteni huo wote ndani yake, kama Yeye alitaka kufanya hivyo. Yeye ni Mungu.” A-ha. Kwa hiyo, hiyo ni kweli. Mungu hufanya yale Yeye atakayo kufanya. Nami ninaamini ya kwamba—ya kwamba—ya kwamba nyangumi alimmeza Yona.

¹⁰¹ Kama vile msichana mdogo alikuwa siku moja akija kutoka maskanini. . .

¹⁰² Alikuwa mdogo, kama maskini huyu mtoto mtukutu jana usiku, ama usiku wa leo, aliyechana nywele zake nyuma hapa, mwajua. Maskini ninii yake. . . Nilifikiri alikuwa mrembo. Maskini yule mwimbaji, sidhani. . . Hana budi kusikia. Natumaini sitaumiza hisia zake.

¹⁰³ Lakini, alikuwa ni mrembo kwelikweli. Basi msichana huyu mdogo alikuwa tu ndio kwanza aokoze, naye alikuwa ameishikilia Biblia yake moyoni mwake, akiimba tu.

¹⁰⁴ Kulikuwako na mzee kafiri aliyeshi upande wa juu ya barabara kule, katika mji mdogo unaoitwa Utica, Indiana. Naye akasema, “Umefurahia nini hivi asubuhi ya leo?”

Akasema, “Vema, ndio kwanza nimpate Yesu.”

¹⁰⁵ Kasema, “Unajua je ulimpata?” Akasema, “Ni kitu gani hicho ulicho nacho mkononi mwako, kitabu cha maombi?”

Akasema, “La. Ni Biblia.”

Kasema, “Nadhani unaiamini Hiyo?”

Kasema, “Ninaamini kila sehemu Yake.”

106 Ndipo kasema, “Unaamini ile hadithi humo ndani kuhusu Yona na nyangumi?”

Akasema, “Naam, bwana. Ninaamini kila neno lake.”

Akasema, “Aa, sivyo ilivyo, kipenzi. Usiamini Hiyo.”

Akasema, “Lakini ninaamini ni hivyo.”

107 “Vema, sasa,” kasema, “utathibitishaje ya kwamba ni ya kweli, nje ya imani, kama mnavyoiita?”

108 “Vema,” akasema, “nitakapofika Mbinguni, nitamwuliza Yona.” Kwa hiyo . . .

109 Naye kafiri huyo akamwambia msichana huyo mdogo, akasema, “Vipi kama Yona hayuko Huko?”

110 Kasema, “Basi itakubidi wewe kumwuliza.” Kwa hiyo hiyo ni karibu tu jinsi ilivyo, mwajua. Ikiwa hakuwako Huko, wanajua mahali alipokuwa.

111 Kwa hiyo, ni kama tu Hiyo ilivyosema. Kama Biblia ilisema ya kwamba Yona alimmeza nyangumi, ningeamini, kama Biblia ilisema hivyo. Kwa hiyo ninaamini ya kwamba mambo hayo yote ni kweli, kila Neno Lake, kila fungu la Biblia.

112 Basi watu wengi wanamkemea Yona. Sasa hebu sisi, kama Wakristo. . . kwa kuwa tunazungumza juu yake, kama mmoja wa jamaa hapa ambao Yesu aliwarejea. Nyuma, miaka mingi kabla ya Kristo, alikuwa ni ishara kwa kizazi hicho. Na hebu tutafakari tu juu yake kwa dakika moja.

113 Huyo hapo, huku mikono yake imefungwa nyuma yake, na miguu yake. Naye nyangumi alikuwa akizungukazunguka majini, akitafuta chakula. Vema, samaki anapokula, tunajua yeye hushuka moja kwa moja chini kabisa na kuzipumzisha, hizo pezi zake, chini ya—ya bahari.

114 Mlishe samakidhahabu wako, kisha umwangelie. Akijaza maskini tumbo lake, atashuka moja kwa moja chini ya gudulia na kupumzika kidogo. Ameshiba, kama tu mnyama mwingine yeyote.

115 Simba wa Afrika, wakati yeye. . . Yeye huzungukazunguka mpaka anapopata chakula, naye ataua chochote. Upesi tu atapata vipande vyake vizuri sana vya nyama, kama chochote kile. Kwa hiyo, lakini wakati yeye—wakati anapokula, ataondoka aende na kulala chini. Nawe ungeweza kutembea moja kwa moja juu yake; asingekusumbua. Huenda akasimama na kunguruma, simba mdogo, ama akufukuze, lakini ameshakula. Hivyo tu. Yeye hutumia nguvu zake kuu kuu tu, ili kula.

116 Na samaki huyo, alipokuwa amekula, alikuwa ameshuka chini kabisa sasa. Naye alikuwa ameshiba kabisa, nadhani, tumboni mwake. Alikuwa na nabii huyu huko chini, tumboni mwake. Nami daima kidogo nilimhurumia, kwa sababu wewe...

117 Watu sikuzote wanazungumza kuhusu, “Vema, Ndugu Branham, nilikuwa na mkono uliolemaa, na nikaombewa, juma moja lililopita. Ndugu *Fulani-wa-fulani*, mchungaji wangu, aliniombea, na kweli sina nafuu hata.” Kamwe hutapata nafuu hata kidogo, mradi tu unauangalia mkono huo. Huwezi kuuangalia mkono. Inakubidi kuiangalia ahadi. Daima unaangalia na kusema, “Vema, nimekuwa na kidonda tumboni mwangu, na kingali kinachoma.” Hilo, hilo halina uhusiano wowote nalo. Inakubidi kuamini. Hicho ndicho kitu kinachofanya uponyaji, ni imani yako. Unaona?

118 Sasa, angalieni. Ati wanena kuhusu dalili? Yona alikuwa na kisa halisi cha dalili. Angalieni hapa. Hebu tufikirie alikuwa amerudi nyuma. Naye yuko katika tumbo la nyangumi, labda fathomu arobaini chini ya bahari, katika dhoruba baharini, na amelala kwenye matapiko yaliyomfika shingoni, akiangalia kote, amezungushiwa majani ya baharini, kila mahali. Ndipo aliangalia *huku*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. *Huko* ilikuwa ni tumbo la nyangumi. *Huku* ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Kila mahali angeweza kuangalia, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Sasa, alikuwa na kisa kizuri cha dalili. Hakuna mtu hapa ndani, mбая hivyo, usiku wa leo. Nina hakika.

119 Lakini mnajua kile Yona alichosema? Alisema, “Hizo ni ubatili udanganyao. Sitaziangalia, bali mara nyingine tena nitaliangalia hekalu Lako takatifu.” Haya basi. Alikataa kuliona tumbo la nyangumi. Alikataa kuziona dalili.

120 Kwa nini? Alijua ya kwamba wakati Sulemani alipoliweka hekalu hilo wakfu kwa Mungu, wakati ile Nguzo kuu ya Moto na wingu liliponing’inia pale nje, Lile (ombi la Sulemani) lilipita juu likaenda na kuchukua mahali Pake pa kupumzikia pamoja na sanduku la agano. Ndipo wakati—wakati Sulemani alipooomba, aliomba, “Bwana, watu Wako popote wakiwa hatarini na watazame kuelekea mlima huu mtakatifu, ama mahali hapa patakatifu, na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Naye Yona alikuwa na matumaini ya kwamba Mungu aliyasikia maombi ya Sulemani, kwa sababu alikuwa ni mtumishi wa Mungu.

121 Na kama angeweza kuwa na kiasi hicho cha imani katika ombi la mtu aliyekuwa akiweka wakfu hekalu la duniani; na mtu, akiomba ombi hilo, ambaye hatimaye, maishani mwake, alirudi nyuma; na chini ya hali hizo za mambo, akiwa na dalili za aina hiyo, angeweza kuwa na tumaini kubwa kama hilo kwamba Mungu angesikia maombi yake; ni zaidi sana vipi sisi

tunavyopaswa, usiku wa leo, ambao tumeketi katika Uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka, kuangalia mbali na dalili zetu, hadi Mbinguni Kwenyewe, ambako Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu, akiwa na Damu Yake Mwenyewe, kufanya maombezi juu ya maungamo yetu! Wakati, maelfu waliotuzunguka na kote ulimwenguni, ambako uamsho mkuu wa uponyaji unapiga sasa, moja kwa moja kwenye saa hii kabisa kuna watu wanaoponywa, kote ulimwenguni. Saa imewadia.

¹²² Sasa, ati tuangalie dalili zetu? Aibu kwetu. Wakati, Yona, na chini ya hali hizo za mambo, angeweza kuangalia mbali na dalili zake. Alisema alikataa kuziangalia. Akasema, “Ni ubatili udanganyao. Nitatazama kuelekea hekalu Lako takatifu.”

¹²³ Ee Mungu, tupe wanaume na wanawake wenye imani ngumu, ambao hawataangalia dalili wala kuangalia chochote ibilisi anachokupa! Mrudishie. Sema, “Ninaamini katika ufufuo wa Yesu Kristo. Ninaamini katika nguvu Zake zinazotosheleza kwa yote. Ninaamini kwamba Uwepo Wake upo hapa sasa kuniweka huru na kifungo chochote ambacho Shetani ameweka juu yangu. Nami ninatazama kwenye . . . Ambapo Yeye ameketi, mkono wa kuume wa Mungu, yu hai milele ili kufanya maombezi kwa ajili yetu.”

¹²⁴ Kwa Damu Yake Mwenyewe, kama Kuhani Mkuu, Yeye ameketi Kule, juu yake. Ni zaidi sana vipi tunavyopaswa kuangalia Mahali Patakatifu pa Mungu, ambapo Yesu Mwenyewe, Mwombezi wetu, Yule pekee aliye kati ya Mungu na mwanadamu, amesimama na Damu Yake Mwenyewe, kutuombea kwa maungamo yetu! Amina. Usichukue. . . *Amina* inamaanisha “na iwe hivyo.” Ninaliamini kwa moyo wangu wote. Angalieni.

¹²⁵ Mnajua kile Mungu alichofanya? Hili ni mshangao kwa wanasayansi. Yeye. . . Sijui kama aliweka tangi la oksijeni kule chini, ama kile Yeye alichofanya, bali mtu huyo alikaa hai siku tatu mchana na usiku, katika tumbo la huyo nyangumi. Sijui alichofanya Yeye. Lakini alimbeba bure, kote kote kutoka Tarshishi, akarudi mpaka Ninawi.

¹²⁶ Nanyi mwajua, wanabiashara wa mji huo, kazi yao kubwa ilikuwa ni kuvua samaki. Basi siku moja wakati. . . Walimwabudu nyangumi, akiwa ni “mungu wa baharini,” mnyama mkali aliye mkubwa kuliko wote baharini. Wakati watu wote walipokuwa wametoka, yapata saa tano siku moja, wakizivuta na kuingiza nyavu zao, huyu hapa “mungu wa baharini” akaja, ambaye walikuwa wamemwabudu. Akakimbia hadi ufukoni, akatoa ulimi wake nje, ndipo nabii akatoka moja kwa moja kinywani mwake. Mungu wao mwenyewe akamtema huyo nabii. Si ajabu walimwamini. Mungu alikuwa ameitoa kwa ajili yao. Na si ajabu walitubu, na kuwavalisha wanyama nguo

za magunia. Waliamini ujumbe wake. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo.

¹²⁷ Angalieni yale Yesu alisema hapa kumhusu Yona, mnaona, kumhusu yeye. Alisema, “Ki—kizazi kibaya na cha zinaa kinatafuta ishara.” Huenda nikaikandamiza imani yenu kidogo hapa, bali ninaamini Yeye alikuwa akirejea kizazi hiki. Nitawaambieni ni kwa nini. Kwa kuwa, tunajua ya kwamba hiki ni kizazi kiovu na cha zinaa.

¹²⁸ Hapajakuwapo na wakati, tangu Sodoma, ambapo ushoga na upotovu ulikuwa ukiongezeka kama ulivyo sasa. Unapaswa kwenda ofisini mwangu na kusoma barua za akina mama kutoka California na kotekote, kuhusu maisha ya wavulana wao. Loo, ni baya sana! Nami nilichukua gazeti hapa, miaka michache iliyopita, nikiruka juu ya Los Angeles, na ambapo lilisema ya kwamba—ya kwamba ile dhambi kuu ya Sodoma ilikuwa imeongezeka sana kule hata ilikuwa imeongezeka asilimia ishirini juu ya mwaka uliotangulia. Na kote kote, hata kwa maafisa wa serikali, na iko kila mahali. Dhambi!

¹²⁹ Ni kwa sababu kwamba wanawake wamejifanya rahisi sana. Wamejiletea hayo wenyewe. Na ni—ni shughuli rahisi. Ilikuwa kwamba, ulivua kofia yako, kwa mwanamke mtaani. Na sasa ungefanya hivyo, angekucheka usoni mwako. Mnaona? Wewe—wewe... Tumejifanya lundo la upotovu, ni kujidhili wenyewe sana.

¹³⁰ Sasa tunaona ya kwamba, tunaona ya kwamba Yesu alisema kwamba, “Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara, na kutakuwako na ishara kitakayopewa. Kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi, siku tatu mchana na usiku, ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika—atakuwa katika moyo wa nchi, siku tatu mchana na usiku.”

¹³¹ Alikuwa akizungumzia kitu gani? Kizazi kiovu na cha zinaa kingeipokea ishara ya kufufuka kwa Yesu Kristo. Na hilo ndilo tunalofanya. Tunajua usiku wa leo kwamba Yeye hajafa, bali yu hai milele, na Yeye yuko pamoja nasi.

¹³² Katika wakati huu wa ulimwengu wa kanisa, na kujiunga na kanisa, na ubaridi, na mambo tuliyo nayo duniani leo hii, na wafuasi vuguvugu wa kanisa, wenye kudhihaki, wakifanya mzaha, “Wakiwa na mfano wa utauwa, huku wakikana nguvu za Roho Mtakatifu,” ambao, tumeamriwa kujiepusha nao. Katika saa iyo hiyo, ya hicho kizazi kiovu na cha zinaa, Yesu Kristo anafufuka, na katika nguvu za kufufuka Kwake, kuthibitisha ya kwamba Yeye yu hai milele, yeye yule jana, leo, na hata milele. Kizazi kiovu na cha zinaa kitatafuta ishara, nacho kitaipata. Kutakuwapo na ishara hii watakayopewa, ya ufufuo. Nafikiri tunaishi kuiona leo hii.

¹³³ Na Yeye anaendelea, kurejea kwa, kizazi cha Sulemani, wakati Sulemani alipojitokeza jukwaani. Sasa, sote tunajua,

kama ndugu wahudumu na wasomaji, kwamba hiyo ilikuwa—hiyo ilikuwa ni, karibu, ule Utawala wa Miaka Elfu Moja, kwa Israeli. Huo ulikuwa ni wakati wa ufanisi wa Israeli. Walijenga hekalu wakati huo. Hawakuwa na vita.

¹³⁴ Sulemani alikuwa mtu mwenye kipaji. Mungu alikuwa amempa karama kuu ya upambanuzi. Na kila mtu nchini, kwa moyo mmoja na nia moja, aliamini katika karama hiyo. Ilikuwa ndiyo jambo lililovuma ulimwenguni, kila mahali. Kila mtu aliwaogopa kwa sababu kwamba—kwamba walijua ya kwamba kulikuwako na Mungu aliye hai miongoni mwao.

¹³⁵ Hivi si ingekuwa vizuri usiku wa leo, kama Marekani yote, kama Marekani yote, ingekubali karama ambayo Mungu ametupa, Roho Mtakatifu, na kwa moyo mmoja tungeafikiana juu yake, na kuiunga mkono, na—na kama vile tu walivyofanya siku ile? Loo, ungekuwa ni wakati wa upeo wa ustawi jinsi gani! Ile karama kuu, “yule Mkuu kuliko Sulemani yupo hapa,” bali hatuipi heshima ambayo waliipa katika siku ya Sulemani.

¹³⁶ Wakati walipoiona karama hii kuu ikitenda kazi katika Sulemani, kila mtu aliamini, kwa moyo mmoja na nia moja. Kabila la—la Yuda, na kabila la Benyamini, na makabila mengine yote, hapakuwapo na tofauti ndani yao. Walikuwa na moyo mmoja na nia moja. Wangekusanyika pamoja, nao wangesema, “Tafakarini tu juu ya Yehova wetu mkuu! Yeye alitutumia karama, nayo inakaa ndani ya mtu.”

¹³⁷ Na yale mambo makuu, mbona, si—sifa za Sulemani zilienea kote ulimwenguni. Na mataifa hayo mengine yalimtolea ushuru, wakamtumia mafahali, ngamia, na zawadi kuu za dhahabu, na—na wakamsaidia na mawe na kila kitu, kulijenga hekalu.

¹³⁸ Hicho ndicho Marekani inachohitaji, usiku wa leo; sio ongezeko jipya kwa siasa; si dhehebu jipya kanisani; si kitu cha namna hiyo. Wanapaswa kuja pamoja katika moyo mmoja, na kuamini na kupokea karama ya Roho Mtakatifu ambayo Mungu ametutumia katika siku hizi za mwisho, ambapo miamsho hii mikubwa ya kimiujiza ya siku za mwisho imeanza kote nchini.

¹³⁹ Lakini, wakati wowote, Mungu anapotuma karama kwa taifa, nalo taifa hilo linaikataa karama hiyo, taifa hilo huingia katika machafuko. Hivi ulijua, yapata miaka hamsini iliyopita, ya kwamba, Urusi, baraka za Kipentekoste zilianza huko Urusi, yapata miaka hamsini ama sabini na tano iliyopita, kabla hazijapata kuja hapa? Hiyo ni kweli. Nao wakazikataa, nanyi mnaona walichopata. Taifa lolote! Angalia Uingereza leo hii; wakati ule uamsho mkuu wa Wesley, yale matengenezo makuu. Angalia mataifa ambamo uamsho mkuu ulianza, nao walipoukataa, kile kilichowafanyikia.

¹⁴⁰ Na taifa lolote litakalopokea baraka ambayo Mungu anatumia, hilo taifa hufanikiwa.

¹⁴¹ Nawaambia. Ninaamini, usiku wa leo, ya kwamba usalama wetu hauko katika kujenga kinga za mabomu ama kitu kama hicho. Ninaamini usalama wetu umetengenezwa kwa manyoya. Chini ya mbawa Zake, tutastarehe. Loo, naam!

¹⁴² Utaingiaje kwenye kinga ya bomu? Moja ya hayo mabomu litalipua maili mia moja na hamsini mraba, na kina cha futi mia tano, ardhini. Mbona, ingetikisa kila mfupa ndani yako, uteguke, kama ungalikuwa huko chini kabisa kwenye lava hiyo.

¹⁴³ Lakini kuna mahali pa usalama, na hapo ni katika Yesu Kristo. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Huo ndio usalama wa mwaminio, chini tu ya mbawa Zake, kudumu salama. Hakika.

¹⁴⁴ Angalieni wakati huu mkuu, laiti watu wameamini tu kile Mungu alichowatumia! Lakini, kukikataa Hicho, ni kuingia katika machafuko. Na hivyo ndivyo tumefanya, kama taifa, tumezikataa baraka za Mungu, na kukibadilisha Hicho na mapokeo. Bali Mungu ametuma shahidi, nao watu wameshindwa kuliona.

¹⁴⁵ Nami nafikiri ya kwamba watu wa Kipentekoste, kadiri ya mambo mengi ambayo Mungu amewatumia, na hata hivyo makanisa yetu yamebaki nusu tupu. Mchungaji hawezi kulifanya mwenyewe. Walei hawana budi kusaidia katika jambo hili. Sisi sote ni wahusika.

¹⁴⁶ Hilo ndilo lililosababisha machafuko mara ya kwanza, kwenye Baraza la Nikea. Walitaka, wakati, “Fundisho la Wanikolai.” *Niko* maana yake ni “kushinda,” na *walei* maana yake ni “kuondoa kutoka kwa washirika, kufanya mtu mtakatifu.”

¹⁴⁷ Huyu si mtu mtakatifu, kilima kitakatifu. Ni Mungu mtakatifu, Mungu mtakatifu miongoni mwa watu. Washirika wana sehemu yake. Sisi ni watoto. Hakuna wakubwa miongoni mwetu. Mnawezaje kuwa na imani wakati mna shauku ya heshima mmoja kwa mwingine? Sisi sote ni mmoja, katika Kristo Yesu. Hamna watu wakubwa na watu wadogo. Sisi sote ni sawa. Sisi ni watoto wa Baba mmoja, na sisi ni watoto Wake.

¹⁴⁸ Sasa tunaona, Mungu amefanya mambo makuu kwa taifa hili. Alimtuma Tommy Osborn, Oral Roberts, na—na watu wengi mashuhuri, kote nchini, wakaning'iniza kila karama ndogo mbele za watu.

¹⁴⁹ Lakini ni kama tu baharia mzee, siku moja, akienda baharini. Mtu huyo alimwambia, maskini baharia huyu... Kamwe hakuwa amewahi... Mtu huyu, mshairi, alikuwa ameandika juu ya bahari, na kuzungumza juu yake, bali kamwe hakuwa ameiona. Kwa hiyo, alikuwa akishuka kwenda ba—baharini. Na, loo, yeye alisema... akakutana na huyo baharia mzee. Naye akasema, “Waenda wapi, mtu wangu mwema?”

150 Akasema, “Chini baharini, kuwasikia shakwe, na kuona mawimbi yake ya bahari, na kuziona anga za samawati zikijiakisi majini.”

151 Maskini baharia huyo akavuta kiko chake, mara nne ama tano, kisha kasema, “Sioni chochote cha kulisimua sana kuihusu. Nilizaliwa juu yake, miaka hamsini iliyopita.” Hakika. Alikuwa ameona mengi sana yake hata yakawa ya kawaida kwake.

152 Hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste leo hii. Utakuja wakati ambapo majaliwa haya yataondolewa kwetu. Ndipo mtayalilia, bali hamtayapata. Mnaona? Mmeona mengi sana.

153 Mwanamke mmoja hapa, sio muda mrefu uliopita huko Louisville, Kentucky. Alikuwa na mtoto mchanga, naye alikuwa akizunguka, maskini mvulana mwenye umri wa miaka miwili hivi, ndivyo ilivyokuwa. Alikuwa amemshika mikononi mwake, naye angeokota vitu vidogovidogo. Angesema, “Angalia, kipenzi, tazama.” Naye mtoto huyo mchanga angeketi tu na kukodoa macho. Angetembea aende kwenye kitu kingine, aseme, “Kipenzi, tazama hiki.” Ndipo watu humo dukani wakaanza kumwanguka. Akaanza kushikwa na mpagao. Na kwa hiyo akachukua kijichacharisha kidogo, ambacho kinapaswa kumvutia mvulana mdogo kama huyo. Kasema, “Tazama, kipenzi. Tazama, tazama, tazama, kipenzi. Tazama, kipenzi, tazama.” Naye maskini mvulana huyo akakodoa macho tu.

154 Ndipo akaanguka kwenye kaunta. Watu wakamjia na kumsimamisha, wajue shida ilikuwa nini. Akasema, “Maskini mvulana wangu,” akasema, “alianza tu kukodoa macho angani.” Kisha kasema, “Nilimpeleka kwa daktari, naye daktari anasema amepata nafuu. Lakini vitu ambavyo vinapaswa kumvutia mvulana mdogo kama yeye havimvutii tena. Anaonekana tu ni kama havioni.”

155 Hicho ni kitu kama kanisa leo hii. Mungu ametikisa kila namna ya karama mbele ya kanisa, ambayo aliahidi kutikisa, na bado tunakodaa macho angani. Mnaona? “Mabwana, tungetaka. . . Bwana, Mwalimu, tungetaka kuona ishara kutoka Kwako.” Mnaona? “Mwalimu, tuna shauku ya hili.” Wakati, Yeye amefanya kila kitu, katika Biblia, alichohidi kufanya. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

156 Na jambo la kwanza mwajua, mtakuja kujua, mnasema, “Vema, hivi haijaandikwa ya kwamba tunapaswa kuwa na Unyakuo?”

157 Na itakuwa kama ilivyokuwa kwa Yohana Mbatizaji. Walisema, “Hivi haijaandikwa katika Maandiko ya kwamba kunapaswa kuwa, kwanza, Eliya kuja?”

Akasema, “Eliya amekuja tayari nanyi hamkujua.”

158 Moja ya siku hizi, hapo Dhiki itakapoanza, mtasema, “Hivi hakukupaswa kuwa na Unyakuo kwanza?”

159 Na utakuwa, “Umepita tayari, nanyi hamkujua chochote kuuhusu.” Mnaona? Utakuja kama mwizi usiku.

160 Nawaambia, wakati umewadia kwa waaminio kutengeneza taa zao, wawe chonjo. Wakati wa kuitwa umewadia. Inatupasa kukumbuka hilo.

161 Sulemani, walimwamini, watu wote, kwa moyo mmoja na nia moja, na si ajabu ujumbe ulienea kila mahali.

162 Lakini, leo hii, kama Mungu akituma kitu fulani, kama kikiligusa dhehebu fu—fulani, kanisa, hayo mengine hayatakuwa na uhusiano wowote nacho. La, bwana. Kama kikiwagusa Wabaptisti, usiwatarajie Wamethodisti kufanya lolote. Kama likigusa Pentekoste, watarajie hayo mawili kukaa mbali, maana hakika watafanya hivyo. Kwa hiyo haya basi. Inategemea kinatoka wapi. Hakina budi kupitia kwenye duru yao la sivy hakifai kitu.

163 Hilo ndilo jambo lile lile walilowazia wakati Mungu alipomtuma Yesu, kwamba ingembidi kumtuma kupitia Mafarisayo, ama Masadukayo, ama baadhi yao. Na Yeye alimtuma kwa hao wote, pasipo kupitia yeyote wao. Hivyo ndivyo Mungu afanyavyo. Yeye ananinii tu... Yeye, mnaona, Yeye kamwe hakuja kwa yeyote wa hao. Alikuwa, akawaita kundi la majoka nyasini. Hiyo ni kweli.

164 Na kwa hiyo tunaona ya kwamba Mungu hufanya mambo kwa njia Yake Mwenyewe. Na sisi hatuwezi kushikilia chochote sana, na kusema, “*Hii* ni sehemu yangu, na wewe huna shughuli. Usipoona kupitia miwani yangu, basi huoni.” La. Mungu anayo miwani kwa ajili yetu kuona kupitia, hiyo ni Roho Mtakatifu. Ndipo inaliona Neno la Mungu na kuliadini Hilo, na inapenda na kushiriki, nayo blanketi liko mbali kutosha kwa ajili ya jirani. Nanyi mnajua ninayomaanisha.

165 Ulimwengu unakufa ukitaka upendo kidogo, na mtu fulani wa kuwajali. Hiyo ni kweli. Wameona mengi sana ya upuuzi huu baridi, mgumu, uliokauka. Lakini, nawaambia, kisa hiki cha mtindo wa kale cha wokovu kitaifanya nguo ya—ya kaliko na nguo ya hariri wakumbatiane. Itafanya koti rasmi na jozi ya surupwenye kuitana “ndugu.” Hakika itafanya. Itakuondolea ugumu moja kwa moja, wakati kweli ukimweka Kristo maishani mwako, kwa njia sahihi. Hakika itaondoa.

166 Sasa, tunaona ya kwamba Sulemani, ule wakati mkuu, kwamba sifa zake zilienea kila mahali katika nchi zote, nao wapita-njia wakasikia habari zake. Wakapeleka katika nchi zingine. Na njia—njia pekee waliyokuwa nayo wakati huo, haikuwa ni televisheni na vitu walivyo navyo siku hizi, na magazeti. Ilikuwa ni kutoka mdomoni hadi sikioni. Nayo misafara yao ingepita, na kupita ikienda, na kufanya biashara,

na kuipeleka kwa mataifa mengine. Na hatimaye sifa zake zikafika huko chini kabisa kupitia jangwa la Sahara, ikaingia mahali paitwapo Sheba.

¹⁶⁷ Inaitwa hapa, “Malkia wa Kusini.” Hebu tuzungumze juu yake, dakika chache. Yeye alikuwa maskini malkia, kafiri. Alikuwa amekuzwa kuabudu sanamu.

¹⁶⁸ Lakini, mnajua, “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno la Mungu.”

¹⁶⁹ Na mle chini kabisa, Neno lilifika, kwamba, “Mungu, Mungu aliye hai, alikuwa akiishi miongoni mwa watu Wake.” Basi maskini moyo wake ukaanza kurukaruka kwa furaha.

¹⁷⁰ Na kila wakati msafiri angepitia kule, aingie kwenye ufalme wake, kufanya biashara, ya kiungo na chochote kilichowabidi kubadilishana, na kadhalika, na vito, mbona, angewaita kwenye kasri, na kusema, “Umepitia Palestina?”

“Naam.”

¹⁷¹ “Ulipitia Israeli. Aisee, nataka kukuuliza jambo fulani. Ni kweli ya kwamba Mungu wao yuko miongoni mwao?”

¹⁷² “Loo, niliiona! Unapaswa. Mbona, hujapata kuona kitu kama hicho. Mungu wao ameshuka na kumtia mafuta mmoja wa ndugu zao, nao wamemfanya kuwa mfalme. Na, loo, hiyo, laiti ungaliuona umoja wa hao watu! Wote wako na moyo mmoja na nia moja. Naye huyo Mungu anawanyeshea tu baraka. Naye ana karama kuu, yenye nguvu ya upambanuzi. Na ananinii tu... Unapokuja mbele yake, imezidi binadamu. Ni—ni ya kimbinguni, jinsi anavyoweza kujua mambo.”

¹⁷³ Maskini moyo wake ukaanza kudunda. “Kuna jambo fulani halisi.” Alitaka kuona hilo. Vema, iliendelea na kuendelea. Muda si muda wajua...

¹⁷⁴ Unajua, imani chanzo chake ni kusikia. Na Mungu anapoanza kushughulika na moyo wa mwanadamu, kuna jambo fulani linalotukia ndani, ambalo kamwe huwezi kulielezea.

Kila siku, akaanza kuona kiu. Alitaka kuliona.

¹⁷⁵ Mwajua, Biblia ilisema, “Heri wenye njaa na kiu kwa ajili ya haki, maana hao watashibishwa.”

¹⁷⁶ Sasa tunaona. Hebu tuliigize tu kidogo, kusudi watoto walipate. Ninaweza kuwazia juu ya siku moja alipokuwa ameamua kwamba alikuwa anaenda kuona kama ilikuwa ni kweli au si kweli.

¹⁷⁷ Hilo ni jambo jema. Vema, kama tulivyosema juu ya Filipino jana usiku, “Njoo, ujionee mwenyewe.”

¹⁷⁸ Alikuwa ameanza labda kununua Bi—Biblia, Agano la Kale, ya ngozi, magombo. Naye akaanza kusoma, kuona alichokuwa Mungu huyu, waliyekuwa wakizungumzia. Aliona jinsi Huyo alivyotenda kazi katika maumbile Yake.

179 Ndipo basi anaona kwamba tabia yenyewe na uhai wa huyo Mungu ulikuwa ukidhihirishwa kupitia mtu, akijitambulisha Mwenyewe kwa watu Wake, kupitia kwa hao watu, yale Yeye aliyoahidi kufanya. Vema, moyo wake ukaanza kuona njaa, kuliona. Kwa hiyo sasa yeye. . .

180 Siku moja, aliwaza kwamba ataenda kuliona, mwenyewe.

181 Sasa, hilo ni wazo jema. Nenda ukajionee, mwenyewe. Usichukue kile mtu mwingine anachosema. Nenda ukajionee. “Yachunguzeni Maandiko,” Yesu alisema, “kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Na Hayo ndiyo Hayo yanayonishuhudia Mimi.” Kile tu Yeye alichosema.

182 Angalieni sasa. Maskini mama huyo, kufanya hivi, alikuwa na pingamizi nyingi sana.

183 Sasa, jambo la kwanza lililombidi kufanya, yeye, kwanza, itambidi aende kwa kuhani wake kafiri aombe ruhusa, kwa sababu alikuwa malkia, mwanamke mwenye heshima. Nalo kanisa la taifa, mwajua, pale, ilimbidi. Ilibidi walitafakari, kwa sababu ilikuwa inaenda kumlazimu ku—kuiacha dini yake mwenyewe, kwenda kuchunguza nyingine ambayo hakujua chochote juu yake, bali alikuwa na njaa ya kujua habari zake. Kwa hiyo ninaweza kuwazia anamwendea baba mtakatifu wa hekalu la kipagani, naye akasema, “Baba Mtakatifu, nina shauku. . . ninasikia ya kwamba huko Israeli wana Mungu m—mkuu kule, ambaye anajitambulisha Mwenyewe kupitia watu Wake. Wanafanya ishara kuu, na maajabu, na miujiza.”

184 Ninaweza kumsikia huyo kuhani akisema, “Sasa, binti yangu, hao si kitu ila kundi la watakatifu wanaojibingirisha. Usiyasikilize hayo. Unaona? Sasa, kama kuna chochote kinachoendelea, kingekuwa papa hapa kwenye kundi letu wenyewe. Unaona yule mungu mkuu wa kike Dagoni na hawa wengine wote hapa? Unaona miungu hawa wakuu tulio nao hapa?” Maskini malkia huyo akatembea, dakika chache.

185 Mwajua, Mungu akianza kushughulika na moyo wa mwanadamu, ni vigumu kumshawishi mtu yeyote kuliacha. Mnaona?

186 Akasema, “Lakini, angalia, bwana.” Akasema, “Wananiambia ya kwamba matokeo yenyewe yanatokea. Kuna jambo fulani linalotukia, kwamba Mungu hutumia midomo ya mwanadamu, pamoja na hekima kuu ambayo ni kubwa kuliko mtu yeyote anayejulikana. Hazitafutiki, nguvu ambazo Mungu ametoa miongoni mwa watu Wake. Na wote wako katika moyo mmoja. Ninataka kwenda kuliona.”

187 “Mbona,” akasema, “wewe, utashusha hadhi yako, kipenzi, kama ukiliacha kanisa hili. Huwezi kuhudhuria uamsho huo. Kwa hiyo, sisi hatuufadhili huo.”

¹⁸⁸ Lakini, unajua, kwa namna fulani, kama—kama—kama moyo wa mwanadamu ukianza kuona njaa kwa ajili ya Mungu, mfadhili au si mfadhili, unaenda, kwa vyovyote vile, unaona, wakati—wakati Mungu anapoanza kushughulika na mwanadamu. Na ninatumaini hamfikirii mimi ninakosoa, bali ninatoa tu hoja. Mnaona?

¹⁸⁹ Sasa angalieni. Jambo la kwanza unajua, mbona, yeye alisema, “Angalia. Sasa, angalia. Nimekuwa kwenye hekalu hili tangu nilipowekwa wakfu hapa kama msichana mdogo. Mama yangu aliwekwa wakfu hapa. Nyanya yangu aliwekwa wakfu hapa. Umeniambia yote kuhusu nguvu za mungu huyo. Umeniambia vitabu vyote ambavyo umesoma kumhusu. Naye hajafanya msogeo hata mmoja. Yote niliyoona, maandishi fulani kwenye karatasi, lundo tu la kanuni za imani zilizokufa. Lakini wananiambia kuna kitu fulani huko juu kilicho hai.” Amina. Nautakia heri moyo wa maskini malkia huyo! “Yote nijuayo ni kanuni fulani ya imani niliyokariri hapa. Sijaona tendo la kitu cha kimbinguni wala chochote kingine. Hakika, kupitia baadhi ya kizazi chetu, kulikuwako na tendo fulani mahali fulani. Ila tu, mhemuko mdogo tu, kutufanya sisi sote kuingia na kuabudu. Lakini wananiambia ya kwamba huyu ni Mungu aliye hai anayeishi ndani ya watu Wake. Nayo *ile* ni sanamu.”

¹⁹⁰ “Sasa, angalia hapa, kipenzi. Nitakutenga na hekalu. Jina lako litaondolewa moja kwa moja kutoka kwenye kitabu kama ukijishirikisha kule. Unaona?”

¹⁹¹ Bali haikuleta tofauti yoyote kwake. Mwajua, yeye alikuwa na pingamizi nyingi sana, lakini imani yake haikuwa na yoyote.

¹⁹² Imani yako haina pingamizi zozote. Sijali iko wapi, kwamba ni nini, haijalishi ni nani anayesema hapana. Mungu akianza kushughulika na moyo huo wa binadamu, aanze kudunda mle ndani, kwamba ni Kweli, nawe uone kwamba ni Kweli, hakuna kitu kitakachokuweka mbali na Yesu Kristo. Kweli. Unaenda, kwa vyovyote vile.

¹⁹³ Kwa hiyo haijalishi ni kanuni ngapi za imani angeweza kukariri, na jinsi alivyoelimika vizuri, na jinsi ambavyo angeweza kusujudu, na jinsi angelala kifudifudi mbele ya sanamu hiyo, hilo halikuleta tofauti yoyote kwa malkia huyo. Alikuwa akimwonea Mungu kiu. Alitaka kujua, na hangeridhika mpaka ajue, yeye mwenyewe. Alikuwa ameona katika Maandiko, hivyo ndivyo Yeye alipaswa kuwa. Lakini, sasa, itafanikiwa? Hilo ndilo jambo linalofuata.

¹⁹⁴ Unaweza kuzungumza juu ya chochote, lakini je! kitafanikiwa? Unaweza kuelezea hisabiti zake zote, lakini je! itafanikiwa? Ndilo jambo linalofuata. Sasa tunaona.

¹⁹⁵ Sasa, jambo lingine lililombidi kukabiliana nalo. Sasa, aliwazia, kama angalipanda kwenda kule. Kumbukeni, jangwa lilikuwa limejaa watoto wa Ishmaeli, nao ni wapanda farasi

hodari kupindukia na wanyang'anyi. Jangwa lote lilijaa wanyang'anyi siku hizo. Vema, maskini mama huyo, aliwaza hili, "Ninakwea kwenda kuona kama ni kweli. Nitachukua sadaka kidogo, na kama ni kweli, nitaliunga mkono. Kama si kweli, ninaweza kurudisha sadaka zangu."

¹⁹⁶ Wapentekoste wanapaswa kumsikiliza mwanamke huyo. Kuunga mkono vitu vinavyowadhihaki? Mnaachilia kipindi chenu cha redio kuanguka, na kila kitu kingine cha watu wenu wenyewe? Vema.

¹⁹⁷ Alikuwa na akili ya kawaida. Akasema, "Kama nikiona ni kweli, inastahili yote kwangu mimi. Bali kama si kweli, basi nitajua si kweli. Nitaenda nijionee mwenyewe. Nami nitachukua..." Akapakia ngamia uvumba, na—na manemane, na dhahabu, na fedha, na viungo vya gharama kubwa, na—na vitu vya thamani kuu. Akapakia ngamia.

¹⁹⁸ Na sasa kumbukeni, hakwenda kwa Kadilaki iliyoyoyozwa. Ilimbidi kusafiri juu ya mgongo wa ngamia, kupitia jangwa la Sahara.

¹⁹⁹ Si ajabu Yesu alisema atasimama katika kizazi hiki, kukihukumu kizazi hiki. Na watu wengine hapa wanaweza kujua jambo lilo hilo likiendelea, na hawatatembea wavuke barabara.

²⁰⁰ Hebu pima ni umbali gani kutoka Palestina, kutoka—kutoka Yerusalemu, kufikia mahali alipokuwa. Unajua iliwachukua muda gani? Miezi mitatu, juu ya mgongo wa ngamia, kupitia jangwa lenye joto kali mno. Naye alikuwa na nini? Matowashi wachache tu na wajakazi wake pamoja naye. Labda ilimbidi kusafiri usiku. Jua la moja kwa moja la jangwa hilo la Sahara ni kali mno, litakuunguza kabisa. Basi ilimbidi kusafiri usiku.

²⁰¹ Lakini, mwajua, kuna jambo fulani kulihusu, kwamba kama moyo wako ukianza kuona njaa na kiu kwa ajili ya Mungu, huchukui tahadhari yoyote kwa hatari au mahali fulani. Daktari huenda akasema utakufa kwa kansa. Lakini kama moyo wako kamwe ukigonga imani katika Mungu, unajua, unasahau yale daktari aliyosema. Moyo wako haujui woga wowote, mradi tu umejawa na imani.

²⁰² Huyo akaenda, akisafiri usiku, siku baada ya siku, siku baada ya siku, akiyasoma hayo magombo. "Sasa hebu tuone kile alichu Yehova, kile alichokuwa, kile alichohidi, na kadhalika, kile atakachokuwa. Nami nitaona kama huyo ni Yeye katika mtu huyu. Ninajua walicho wanadamu. Na ninaamini nitajua kile alichu Mungu, kwa sababu nimesoma kile Yeye alichokuwa."

²⁰³ Na hebu niseme hili kwa Tucson usiku wa leo, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli. Hawezi kubadilika. Watu hubadilika. Wakati hubadilika. Bali Yeye ni Mungu asiyebadilika, akiwa na Ujumbe usiobadilika. Hauwezi kubadilishwa na kanuni za imani. Hauwezi kubadilishwa na

misimamo ya kimadhehebu. Hauna budi kuwa ni nguvu za kufufuka kwa Yesu Kristo katika Kuzaliwa upya, kwa Roho Mtakatifu. Hayo ndiyo masharti ya Mungu. Hakuna kitu pungufu wala cha zaidi, ila huo.

²⁰⁴ Sasa tunaona, hatimaye, baada ya shida za—zake zote na kadhalika; moyo wake, ukiona kiu. Basi alipoanza kuukaribia mji wa Yerusalemu, ninaweza kuona macho yake yakichangamka. Ndipo akaweka yale magombo kando, kisha akapiga kambi papo hapo nje, labda kwenye lango la ikulu mahali fulani, akijiandaa kwa ajili ya mkutano. Sasa, labda alifika kwenye majira ya jioni.

²⁰⁵ Kesho yake asubuhi, mapema, alienda kanisani ambako mchungaji alikuwa anaenda kuzungumzia. Basi wakati alipokuja kanisani, aliona watu wote wakichukua mahali pao, kisha muziki ukaanza kucheza. Na baada ya kitambo, Mchungaji Sulemani akajitokeza. Labda alipata kiti huko nyuma kabisa upande wa nyuma ya kanisa, bali alikuwa tayari kukaa, aone kitakachosemwa.

²⁰⁶ Hakuwa kama watu wa siku hizi. Ukisema jambo moja ambalo halininii. . . mtu fulani hakubaliani nalo, hawana subira urefu wa sekunde moja. Mnaona? Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu hawafikii mahali popote. Lakini yeye alitaka kuridhika. Sasa, yeye hakuja kusema, “Nitaenda tu huko juu,” kama watu wafanyavyo siku hizi, “na neno la kwanza mwinjilisti huyo asemalo, ambalo kidogo ni kinyume na yale ninayoamini, nitasimama na kuondoka.” Mnaona? Vema, labda wanafanya hivyo. Mnaoa? Lakini inaonyesha kulelewa vibaya, kwanza, na inaonyesha tabia mbaya. Lakini, hata hivyo, watu hufanya hivyo siku hizi. Kwa sababu, wanajisikia si lazima wafanye hivyo. Haiwalazimu. Lakini huna budi kukutana na Mungu, na itakulazimu kujibu.

²⁰⁷ Sasa tunaona ya kwamba mwanamke huyu, alipata, alikuja, sio tu kukaa kwa ujumbe mmoja, alikuja kukaa mpaka ashawishike kama ilikuwa ni kweli ama ni uongo. Basi akachukua mahali pake, naye akangojea.

²⁰⁸ Ndipo basi wa kwanza kuja mbele ya Sulemani. Aliona ya kwamba hekima ya huo utambuzi ulimwambia mtu huyo siri zote hasa za moyo. Moyo wake ukaanza kudunda. Alijua ya kwamba kulikuwako na jambo fulani halisi. Ndipo swala lililofuatia pale, lilikuwa ni jambo lile lile. Ndipo akaanza kuona kiu, mwenyewe.

²⁰⁹ Alikuwa na shida nyingi, Maandiko yanatwambia, alizotaka kujua habari zake. Basi wakati akija, hatimaye, labda alipata kadi ya maombi. Labda namba yake iliitwa, tungesema, kwa kusema tu. Lakini wakati alipofika mbele ya Sulemani, vyovyote vile ilivyokuwa, wakati alipofika mbele ya Sulemani, Biblia ilisema ya kwamba hakuna kitu ambacho hakikujulishwa kwa

Sulemani ambacho yeye hakumfunulia. Mambo yote aliyokuwa nayo, yaliyofichwa moyoni mwake, Sulemani aliyafunua kwa Roho wa Mungu. Basi wakati alipoona hili likitukia, karibu u—uhai wote umtoke maskini malkia huyo.

²¹⁰ Akasimama miongoni mwa watu hao, na akasema, “Bwana Mungu wa Israeli na abarikiwe. Bwana Mungu na abarikiwe Yule ambaye amewachagua Israeli kuwa watu Wake, na ameweka Roho Yake juu ya mfalme Wake na ameonyesha hekima hii.” Kasema, “Wamebarikiwa watu walio pamoja nawe wakati wote, wanaoona karama hii mashuhuri ikitenda kazi. Umebarikiwa wewe, na kukuona.” Alitaka, hata, kuchukua baadhi ya mavumbi kutoka—kutoka Israeli ayapeleke nchini mwake. Alishawishika kabisa kwamba ilikuwa ni Mungu. Ndipo akasema, “Yote ambayo nimeambiwa kuihusu, ilikuwa vigumu kwangu kujua kama niyaamini ama la. Ila sasa nimeiona ikitenda kazi juu ya wengine, na sasa imetenda kazi juu yangu, nami najua ya kwamba ni kweli.”

²¹¹ Si ajabu Yesu alisema, “Atasimama katika Siku ya Hukumu na kukihukumu kizazi hiki kwamba kimekosea. Na, tazama, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa.” Sulemani alikuwa mtu mwenye karama ya upambanuzi. Sasa, Yesu Kristo yupo hapa katika umbo la Roho Mtakatifu, pamoja na—pamoja na karama zote za Kiungu katika mwili wote wa Kristo, akidhihirishwa. Vitu vyote alivyoliahidi Kanisa, tunaonyeshwa sisi.

²¹² Na baadhi yetu hatujali kabisa. Wengine wetu ni kwamba: tunaendelea kutazama mbele. Mradi tu Shetani anaweza kukufanya uangalie mbele kwa kitu fulani huko mbali, unapita juu ya kitu kile hasa ambacho Mungu amekupa wewe.

²¹³ Sikilizeni tamshi hili. “Mwanadamu daima anamsifu Mungu kwa yale amefanya, na kutazamia mbele kwenye kile atakachofanya, huku akipuuza kile anachofanya.” Hiyo ndiyo hali ya mwanadamu. Daima amefanya hilo, na ni jambo lilo hilo usiku wa leo. Wadamu huangalia mbele, na kuangalia nyuma, na kuona kile Mungu afanyacho; na kuzungumza juu ya Mungu mkuu huko nyuma kwenye Pentekoste, na kutazamia Siku kuu ya ule Utawala wa Miaka Elfu wakati Yeye atakapokuja tena, na kupuuza Uwepo Wake wenyewe mbele ya watu Wake, akijiandaa kwa ajili ya Utawala huo wa Miaka Elfu. Wanalipuuza. Ni tabia tu ya watu kufanya hivyo.

²¹⁴ Shetani anakuja miongoni mwao, kuyaficha macho yao kutoka kwenye kitu chenyewe ambacho Mungu aliwatumia. Hivyo tu ndivyo inavyombidi kufanya. Wewe nenda kanisani kadiri utakavyo kuenda, fanya lolote utakalo, lakini kupuuza mambo yenyewe ambayo Mungu anatumia, mbona, tume—tumekataa—tumeyakataa.

²¹⁵ Ni kitu gani kilichomfanya maskini mwanamke huyo kusema hilo? Aliona kitu halisi. Aliona kitu ambacho hakikuwa

tu ni lundo la kanuni za imani. Aliona kitu kilichodhihirishwa na kilikuwa halisi.

²¹⁶ Kwangu mimi, chochote kilichothibitishwa kuwa ni halisi, ni halisi. Nafikiri, leo hii, kwamba ulimwengu mzima unapaswa kuvutiwa. Kama tunaamini ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho, na tunaamini ya kwamba Kuja kwa Bwana Yesu kumekaribia, tunapaswa kuvutiwa hasa na mambo yanayoendelea ya siku hii. Tunapaswa kuyachunguza kwa Neno la Mungu. Kwa sababu, tutaangukia papo hapo, itakuwa imepita nasi hatutajua lolote kulihusu. Hivyo ndivyo imekuwa daima.

²¹⁷ Hao watu hawakuwajua wale watakatifu mpaka walipokuwa wamekufa. Kamwe hawawatambui manabii mpaka walipokuwa wamekufa. Yesu alisema, “Enyi wanafiki.” Kasema, “Jinsi mnavyoyapaka chokaa ma—makaburi ya manabii, nao baba zenu ndio waliowaweka mle.”

Kamwe hawakumtambua Mtakatifu Patrick mpaka alipokuwa amekufa.

²¹⁸ Joan wa Arc, kamwe hawakumtambua kwamba ni mtakatifu. Kanisa Katoliki lilimchoma moto, kwenye nguzo, kama mchawi, kwa sababu aliona maono. Na kumwita mchawi, na kumchoma mwanamke huyo, kwenye nguzo, akilia apate rehema. Mamia machache ya miaka baadaye, waligundua kwamba alikuwa ni mtakatifu. Hapana shaka, walifanya vitubio. Waliichimbua mifupa ya makasisi hao na kuitupa mtoni. Vitubio. Bila shaka.

²¹⁹ Hupitia moja kwa moja juu ya kichwa chao, nao hawajui. Mungu hulifanya hivyo, apate kuwatoa watoto Wake wateule, na kuleta hukumu juu ya ulimwengu unaolikataa Neno Lake na kuukataa Uwepo Wake.

²²⁰ Hebu waangalieni wahudumu hao wote katika siku hiyo, wakiangalia karama ya Mungu katika Yesu Kristo, na kusema, “Ilikuwa ni ibilisi. Sio lazima tumsikie Yeye. Makuhani wetu hawakubaliani na Hilo.” Wako wapi usiku wa leo?

²²¹ Basi mwangalie maskini mwanamke yule mwenye sifa mbaya, maskini Mbegu hiyo ya Mungu iliyochaguliwa tangu zamani ikiwaka moto moyoni mwake. Ndipo mara tu Hilo lilipomulika kote, alisema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii, nami najua Masihi yuaja kufanya jambo hili,” unaona, mara jambo la kwanza lilipomulika, maskini Mbegu hiyo iliyochaguliwa tangu zamani moyoni mwake.

²²² Jina lake liliwekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Vivyo hivyo na lako, kama kamwe litawahi kuwa Mle. Unaona? Hiyo ni kweli.

²²³ Na punde tu hiyo nuru ilipokuja pale! Naye alijua ya kwamba hiyo ilikuwa ndiyo saa waliyokuwa wakiitazamia, Masihi, na hilo ndilo alilopaswa kufanya. Basi alipoona hilo

likitukia, alijua ilikuwa ni Masihi basi, naye hakumwuliza swali tena. Akakimbia mjini, na kusema, “Njoni, mmwone Mtu aliyeniambia mambo niliyofanya. Si hiyo ndiyo ishara yenyewe ya Masihi?” Aliona kitu halisi.

224 Maskini malkia huyo aliona kitu halisi. Hubadilisha mioyo ya watu.

225 Inanikumbusha. Kama ninyi nyote mnavyojua, na—napenda kuwinda. Nilikuwa nikiwinda, milimani huko Mashariki. Katika kufunga sasa, ninataka tu kuwaambia hili. Tukio dogo lililitukia. Loo, na—napenda machweo ya jua. Ninapenda maumbile. Ninapenda kusikia wito. Wanawaua mbwa mwitu wote na kadhalika. Jinsi ninavyopenda kuwasikia wakitoa vilio! Ni—ni—ni—ni. . . Kitu fulani tu kulihusu! Ninapenda hilo. Pia ninapenda mambo ya nje, kilindi kikiita kuingia kwenye Kilindi. Ni Mungu, kwangu mimi. Kusikia kunong’oneza kwa misonobari, na mlio wa ndege, ni Mungu ndani yake, kwangu mimi.

226 Sasa angalieni. Nilikuwa nikienda huko juu kuwinda pamoja na jamaa jina lake Bert. Alikuwa mwindaji hodari. Haikukubidi kuwa na wasiwasi juu yake. Alikuwa mlenga shabaha hodari sana na mwindaji mzuri, na haikukubidi kuhofu kuhusu yeye kupotea. Alijua mahali alipokuwa.

227 Nilifika huko juu nimechelewa, mwaka mmoja, kuwinda pamoja naye. Kuna kosa moja tu nililopata na Bert. Alikuwa ni mwindaji mzuri, bali alikuwa mtu katili kuliko wote niliyepata kukutana naye maishani mwangu. Alikuwa na macho kama ya mjusi, hayo, kidogo ni kama macho yaliyoelekea upande, mwajua, kama vile baadhi ya wanawake wanavyoyapaka rangi macho yao siku hizi, kote, kwa namna fulani kama paka, naye alikuwa nayo. Alikuwa na macho kama hayo, mwajua, kidogo macho yaliyoonekana ya kuchekeka. Naye alikuwa katili sana. Alikuwa akiwapiga risasi watoto wa kulungu ili tu kunifanya nijisikie vibaya. Naye alikuwa akiniambia, “Aa, ninyi wahubiri ni kundi lenye woga kama kuku,” Mnaona?

228 Nami nikasema, “Bert, kama sheria inasema unaweza kumwua mtoto wa kulungu, hiyo ni sawa, maana u—ukubwa au jinsia ya mnyama haijalishi kama sheria inasema unaweza kumwua.” Mnaona? Nikasema, “Hakuna kitu kuhusu kumwua mwana-kondoo. Ibrahimu alimchinja mwana-kondoo na akamlisha Mungu. Hiyo ni sawa.” Nikasema, “Hamna kitu kuhusu kumwua mtoto wa kulungu. Lakini, Bert, wewe unafanya hivyo ili tu kuwa katili. Unampiga risasi mmoja, halafu unampiga risasi mwingine, halafu unampiga risasi mwingine. Huo ni ukatili. Si haki kufanya hivyo. Hayo ni mauaji.”

229 Akasema, “Aa, Billy, jirudie. Wewe ni mwoga kama kuku kama wahubiri hao wengine.” Loo! Alikuwa katili.

²³⁰ Lakini siku hiyo nilipopanda kwenda kule, mke wangu alikuwa pamoja nami. Tukaenda kwenye kibanda kidogo, kulala kule, nao wanawake, na kujiandaa. Basi mimi na Bert tukaondoka asubuhi hiyo. Daima tulibeba the—the—themosi iliyojaa chokoleti moto, na sandwichi. Nasi tungewinda mpaka yapata adhuhuri, ndipo tungetengana, kupanda juu ya Safu ya Rais, na Mlima Wilson, Mlima Adams, na kadhalika. Halafu tungetengana na kurudi na kuingia kambini usiku huo. Tuliwinda kulungu mkiamweupe, kulungu mzuri kweli. Kwa hiyo sisi. . .

²³¹ Mwaka huo, yeye aliniambia, tulipoondoka asubuhi hiyo, kasema, “Hei, Billy, nina cha kukushangaza. Nitawapata mwaka huu.”

²³² Nikasema, “Ni kitu gani hicho, Bert?” Akaingiza mkono mfukoni mwake na kutoa filimbi ndogo aliyokuwa ametengeneza, ilisikika tu kama maskini mtoto wa kulungu akimwita mama yake. Mwajua, maskini mtoto wa kulungu akiita, maskini ile sauti “hwii” anayotoa.

Nikasema, “Bert, usingetumia kitu kama hicho.”

²³³ Akasema, “Aa, haya basi. Ungali una woga kama kuku, siyo?” Na hivyo basi tukaendelea.

²³⁴ Nao msimu huo ulikuwa kidogo umeenda sana. Hao kulungu mikiamyeupe, wanaporushiwa risasi, mara chache, loo, jamani! Wewe nena kuhusu kujificha! Houdini alikuwa ni mwanafunzi. Kwa hiyo jinsi wanavyoweza kujificha! Na kwa hiyo basi tu—tuliendelea mpaka saa tano. Kulikuwa na yapata inchi sita za theluji chini. Hata hatukuona mburuzo. Walikuwa kweli wamejificha vizuri.

²³⁵ Kwa hiyo, yapata karibu saa tano, saa sita, kidogo kulikuwako na mkondo wa barafu, na mahali pa wazi, kitu kama ukubwa wa chumba hiki hapa. Naye Bert alikuwa tu mbele yangu. Aliinama tu chini namna *hii*, na akaanza kuingiza mkono kwenye koti lake hapa. Nami nikafikiri angeninii, tungekula sandwichi yetu, na kisha tutengane na kurudi kambini, turudi usiku huo. Alikuwa akipapasapapasa nyuma. Nilifikiri alikuwa anatoa chupa yake, mwajua, yenye chokoleti yake yenye moto, kwa hiyo nikanyosha niitoe yangu. Basi nilipofanya hivyo, alitokea na hii filimbi ndogo.

²³⁶ Akaniangalia kwa hayo macho ya mjusi, mwajua, kisha akaweka hiyo filimbi ndogo kinywani mwake, namna *hiyo*. Na akaipuliza, kama tu mtoto wa kulungu, ama jamaa mdogo akimwita mama yake. Ndipo wakati alipoipuliza filimbi hiyo, upande wa pili tu wa upenyo huo, mama kulungu mkubwa, kulungu jike, likasimama. Huyu ni mama kulungu. Akaruka juu. Alisikia mlio huo wa mtoto. Ningeweza kumwona akiniangalia, namna *hiyo*, na kutabasamu. Nikawaza, “Bert, hutafanya hivyo.

Hakika hutafanya.” Naye akakiinamisha kichwa chake chini. Akapiga tena.

²³⁷ Ninaweza tu kuona masikio yake makubwa, hayo macho makubwa ya hudhuru. Akatoka moja kwa moja nje kwenye huo uwazi. Sasa, hilo ni jambo la kigeni kwa kulungu kufanya hivyo, hasa sana wakati huo wa mchana, na moja kwa moja wakati msimu wa kuwinda unaendelea, kutoka nje namna hiyo. Lakini alitoka moja kwa moja akaingia katika huo uwazi, konde dogo, konde dogo. Hilo si kawaida kabisa kwake kufanya hivyo. Lakini ni kwa nini alifanya hivyo? Alikuwa mama. Yeye kwa kweli alizaliwa mama. Na mwito huo wa mtoto wake, yeye hakufikiria juu ya hatari. Alikuwa akifikiria juu ya mtoto wake.

²³⁸ Nami nilipomwona akigeuka upande; Bert, nilimsikia akishusha komeo kwenye hiyo .30-06, naye alikuwa hodari wa shabaha. Nilimwona akiamka na kuweka kipini cha darubini hiyo kimelenga kikamilifu moyo wake mwaminifu.

²³⁹ Nikawaza, “Bert, unawezaje kufanya hilo? Unawezaje kulifanya? Hakika hutalifanya.” Nikawaza, “Mama huyo, akijitokeza pale kumsaidia mtoto wake, halafu utaulipua moyo huo mwaminifu kutoka kwake. Unawezaje kufanya hivyo, Bert?” Nami nikasimama pale.

Nikamwona amejituliza, akilenga shabaha namna hiyo.

²⁴⁰ Nikawaza, “Loo, jamani! Si—siwezi kuangalia hilo.” Nikawaza, “Huyo mama, hawezi kujizuia.” Yeye hajifanyi mwerevu. Hafanyi maigizo. Yeye ni mama, ndani yake. Se—se—sehemu yake, ndani yake, yeye ni mama. Na huyo alikuwa ni mtoto mchanga akiita, yuko taabuni, naye anamtafuta.

²⁴¹ Ndipo wakati komeo liliposhuka, yule kulungu akageuka na kumwalia yule mwindaji, kwa kuwa alikuwa ameinuka. Hilo bado halikumsisimua. Alikuwa tayari kufa. Yeye. . .

Loo, laiti watu wanalikuwa tu namna hiyo!

²⁴² Nikageuza kichwa changu. Nisingeweza kumwalia akimpiga risasi. Nikageuza kichwa changu. Nami nikaanza kuomba, kimyakimya, maana nilijua angenikemea kama ningalijaribu kumfukuza. Ni—nikageuza kichwa changu namna *hiyo*, na kusema, “Baba Mungu, msaidie. Msaidie. Usi—usimwache amwue huyo mama, anayekaribu kumtafuta mtoto wake, naye akilia namna hiyo. Usi—usimwache amwue.” Nami nilikuwa nikigeuka, namna *hii*, ndipo nikaona.

²⁴³ Nilikuwa nikisikiliza, niisikie bunduki hiyo ikifyatuka, dakika yoyote, bali bunduki haikufyatuka. Nilingojea na kungojea. Basi nilipogeuka, kuona, yeye alikuwa ameshika namna *hii*. Nilion bunduki hiyo ikienda *hivi*.

²⁴⁴ Akageuka, akaniangalia, na kutoka kwenye hayo macho ya mjusi yaliyoonekana katili, machozi yalikuwa yakidondoka kutoka mashavuni mwake. Akaitupa bunduki chini. Akanishika

kwenye mguu wa suruali. Akasema, “Billy, niongoze kwa Yesu huyo unayemjua.” Papo hapo kwenye lundo hilo la theluji, nilimwongoza huyo mwindaji katili kwa Yesu. Yeye ni shemasi katika kanisa la Kibaptisti huko juu sasa.

²⁴⁵ Kwa nini? Ilikuwa ni kitu gani? Haikuwa ni mahubiri. Ha—ha—haikuwa ni nyimbo alizosikia. Lakini aliona kitu fulani ambacho hakikuwa kujifanya, kitu ambacho hakikuwa ni maonyesho. Aliona kitu kilichokuwa halisi. “Wakinyamaza, mawe yatapiga kelele.” Aliona ya kwamba kulikuwako na kitu fulani mahali fulani ambacho kingeweza kumtuma mtu akakabiliane na mauti, upendo ambao ungeweza kumpeleka huyo mama kulungu akakabiliane na mauti, na hata hivyo asiogope kufa, kwa sababu upendo wa mtoto wake unaita. Alitaka kujua kama kulikuwako na—na Mungu ambaye angeweza kumpa upendo wa aina hiyo, naye akaupata siku hiyo.

²⁴⁶ Enyi marafiki, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa. Yesu alisema wakati mmoja... Iliandikwa katika Biblia, hasa, “Je! mama anaweza kumsahau mtoto wake anayenyonya?” Kasema, “Huenda akafanya hivyo, bali siwezi kuwasahau. Majina yenu yamechorwa kwenye vitanga vya mikono Yangu.” Nayo yamechorwa, kwa alama za misumari mikononi Mwake.

²⁴⁷ Tunatazamia. Hakika, wanaume na wanawake wanaomwamini Yeye, wanatazamia kuona kitu kilicho halisi. Hivi hamngetaka, usiku wa leo, kuwa Mkristo kadiri yule kulungu alivyokuwa mama? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Yeye hakuwa tu mama bandia. Alizaliwa, mama. Kulikuwako na kitu fulani ndani yake, hata hakuogopa chochote, kwa sababu kilimwita atoke. Laiti tungalikuwa tu Wakristo kiasi hicho, kama vile alivyokuwa mama! Ni wangapi wangetaka kuwa na ujuzi huo? [“Amina.”] “Mungu, nijalie niwe tayari, nikiwa na uaminifu kwa Yesu Kristo, kutembea usoni pa ukosoaji, kutembea usoni pa chochote kile, na kuonyesha upendo wangu kwa Mungu. Haijalishi kama ninii yangu—kama watu wangu wakinikataa, kama kila mtu akinicheka, kama kila mtu akiniita wa mtindo wa kale, ama chochote wafanyacho, jalia nionyeshe upendo wa Yesu Kristo moyoni mwangu, kwa uaminifu kama vile yule kulungu alivyoweza kuonyesha umama.” Unataka hilo moyoni mwako? [“Amina.”]

Sasa inamisha kichwa chako na tuombe.

²⁴⁸ Baba wa Mbinguni, aliye mkuu kuliko Sulemani yupo hapa. Upendo mkubwa upo hapa kuliko upendo wa ile hadithi ndogo pale ya yule mama kulungu siku ile. Jinsi alivyokuwa tayari kukabiliana na yule mwindaji, kuikabili ile bunduki, wakati alijua, kwenye dakika yoyote, moyo wake ungelipuliwa kutoka kwake. Lakini, Ee Mungu, wakati mwanamume ama mwanamke, au hata mnyama, yuko tayari kuonyesha upendo!

Ninaomba, Baba, ya kwamba kila mtu hapa ndani usiku wa leo atapokea upendo wa namna hiyo, hata upendo mkuu kuliko huu. Jalia wasione aibu kumkubali Yesu kama Mwokozi wao. Jalia wasione aibu kwa yale Yeye amewatendea. Jalia yeye... kamwe wasione aibu kumkiri Yeye kama Bwana na Mwokozi. Jalia kamwe wasione aibu kumkubali Yeye kama Mponyaji wao, kwa kuwa imeandikwa, “kwa mapigo Yake sisi tuliponywa.”

²⁴⁹ Mungu, naomba uje usiku wa leo na uwe halisi sana kwetu, hata tutaona onyesho la Mungu miongoni mwetu, kwa njia kwamba, hata tutajua ya kwamba Yesu Kristo, Bwana aliyesulubiwa, amefufuka kutoka kwa wafu na amesimama miongoni mwetu. Baba, ninaamini, kama Wewe utafanya hivyo mara nyingine tena, mbele ya watu usiku wa leo, na kujionyesha Mwenyewe hai katika karama kubwa kuliko aliyokuwa nayo Sulemani! Ni karama ya Roho Mtakatifu kwa Kanisa. Ndipo, wanaume na wanawake humu ndani, Baba, watafutwa Kwako. Ninayakabidhi yote Kwako sasa, Baba, pamoja na hadithi hii ndogo na rahisi ya Biblia, na ya ziara ndogo ya kuwinda siku hiyo ya Novemba kule juu kwenye Milima Myeupe. Yote ni Yako sasa, Baba, basi Wewe twaa mamlaka kuanzia hapa. Ninajakabidhi Kwako, na kusanyiko hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²⁵⁰ Sasa, marafiki Wakristo, ikiwa Bwana wetu Yesu ataonyesha upendo Wake kwenu, kwamba Yeye anawapenda, na atakuja miongoni mwetu usiku wa leo, na atathibitisha ya kwamba Yeye yupo hapa, ni Yeye. Sasa, mtu yeyote anajua, kama tulivyosema. Ungejuaje ilikuwa ni Yesu? Unaona? Ungejuaje hilo? Mti fulani huu, ulionekana kana kwamba ulikuwa ni mkuyu, na ikiwa ulikuwa ukizaa mapichi, ungekuwa ni mti wa aina gani? Ungekuwa ni mpichi. Uhai ndani yake ungezaa mapichi. Na kama wewe ni M—Mkristo, Uzima wa Yesu Kristo uko ndani yako, kwa maana ni Roho Mtakatifu. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Na halafu Roho Mtakatifu...

²⁵¹ Kama ningalikwambia ya kwamba roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu usiku wa leo, ungenitarajia kuwa na bunduki, na niwe hapa nje na kuwa mnyang’anyi kama yeye alivyokuwa. Kama ningaliwaambia roho ya mwanasanaa fulani mashuhuri ilikuwa ndani yangu, mngenitarajia kuweza kuichora milima hii hapa jinsi tu inavyoonekana, maana roho ya mwanasanaa huyo iko ndani yangu. Na kama nikiwaambia kwamba Roho ya Kristo iko ndani yangu, Yeye alisema, Mwenyewe, utazifanya kazi za Kristo. Yohana Mtakatifu 14:12 ilisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya; kazi kubwa kuliko hizi, atazifanya.”

²⁵² Nililinkuu hilo wakati mmoja. Mtu huyo akasema, “Hakika, tunafanya kazi kubwa zaidi. Tunahubiri Injili ulimwenguni kote. Hakufanya hivyo katika siku Zake.”

253 Nikasema, “Nionyeshe tu kazi alizofanya, kwanza, na kisha tutazungumza juu ya zilizo kubwa zaidi.” Mnaona?

254 Asilimia tisini ya ulimwengu karibu haijui kitu kumhusu Yesu Kristo. Mamilioni wanakufa kila mwaka, ambao hawakupata kusikia Jina Lake. Zaidi. . . Umezaniwa uinjilisti mdogo leo hii kuliko ulivyowahi kuwa. Hakika. Halafu wananena kuhusu, “Kazi kubwa zaidi,’ kuhubiri Injili.” Sivyoo hakika.

255 Sasa, kuna kadi za maombi, nadhani, zilizotolewa leo. Nadhani walitoa kadi za maombi. Na. . . [Mtu fulani anasema, “Naam.”—Mh.] Vema. Billy? Hayuko hapa? Labda alitoka nje.

256 Vema, wana kadi zozote za maombi kutoka jana? Inua mkono wako, zingine zilitolewa jana, mlipata. Vema, tutaanza nazo. Hebu tuone, tulianzia wapi? Tulianzia wapi jana? Namba moja, ilikuwa hiyo? Namba moja hadi yapata kumi ama kumi na tano? Vema.

257 Hebu tuligeuze, twende mahali pengine basi. Tunataka kumfikia kila mmoja wao. Lakini hebu tubadilishe, mahali pengine. Hebu tuchukue kuanzia. . . Hebu tuchukue zile kumi na tano za mwisho, kuanzia themanini na tano hadi mia moja. Ni nani aliye na kadi ya maombi themanini na tano? Inua mkono wako.

258 Ngoja. Huenda kukawa na themanini na tano mbili. Hizo za kwanza zilikuwa nini? A, sivyoo? [Ndugu wawili wanasema, “A.”—Mh.] A.

259 A, themanini na tano. Ina A kwenye kadi, na themanini na tano. A, themanini na tano. Inua mkono wako. Kadi ya maombi A, themanini na tano. Huyoo mama yupo hapa? Vema. Njoo *hapa*. Themanini na sita, inua mkono wako. Themanini na saba.

260 Sasa, ikiwa huwezi kusimama, tutaona. . . Mabawabu watakuleta moja kwa moja hapa namba yako ikiitwa.

261 Themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa. Tisini. Hebu tuone, sasa, kuna mmoja, wawili, watatu, wanne, watano. Tisini, tisini na moja, -mbili, -tatu, -nne, -tano, hadi mia moja. Fanyeni mstari upande huu *hapa*, mpaka mia moja.

262 Sasa, kama—kama wote hawapo, na mtu fulani anayo kadi, sasa, shikilia tu kadi yako, iweke tu. Karibuni, ninajaribu kuwafikia.

263 Sasa, wakati mkiangalia huku, sasa, angalieni kwa makini sana sasa. Ninawatakeni msikilize kwa makini yale ninayosema. Kadi yako ya maombi haina uhusiano nalo, ni kuwaweka tu katika mstari hapa juu. Hiyo haimaanishi utaponywa. Unaponywa tu, sio kwa kadi ya maombi, bali kwa imani. Hiyo ni kweli. Ni wangapi wamewahi kuwa mkutanoni na wanajua ya kwamba kuna kumi kwa mmoja wanaoponywa huko nje kwenye kusanyiko kuliko wanaoponywa hapa, hapa juu

jukwaani? Hakika ndivyo ilivyo. Ni imani yako. Imani yako. Hii ni kufanya tu mstari wa maombi uanze, hivyo tu, kufanya mstari wa maombi.

²⁶⁴ Sasa angalieni. Kila mtu amefundishwa desturi hii. Nami ninalisema kwa ndugu zangu. Na ambalo ni sawa. Ni Maandiko. Lakini tunataka kuwekeana mikono. Mliona hilo? Lakini hilo halikutolewa kwa Mataifa. Hivyo sivyo Mataifa walivyolikubali.

²⁶⁵ Wayahudi, kumbukeni, Yairo alisema, “Njoo ukaweke mikono Yako juu ya binti yangu naye ataishi.” Hiyo ilikuwa ni desturi ya Kiyahudi. Hiyo ni kweli? “Weka mikono Yako juu ya binti yangu naye ataishi.”

²⁶⁶ Bali Mmataifa alisema, “Sistahili kwamba Wewe uje chini ya paa langu. Sema tu Neno, hivyo tu. Mtumishi wangu ataishi.”

²⁶⁷ Naye Yesu akageuka akasema, “Kamwe sikuona imani kama hiyo katika Israeli.”

²⁶⁸ Akasema, “Mimi ni mtu chini ya mamlaka. Wakati mimi . . .” Naye alitambua nini? Kwamba kila ugonjwa ulikuwa chini ya mamlaka ya Yesu Kristo. Yote yaliyompasa kufanya ni kunena Neno.

²⁶⁹ Na Yeye tayari amelinena. Mnaona? Na hilo ndilo ninalojaribu kuwafanya ninyi watu kutambua.

²⁷⁰ Sasa, watu wengi wanafikiri ya kwamba inakupasa kungojea mpaka mwinjilisti fulani mashuhuri kama, loo, Ndugu Osborn . . . Na Ndugu Osborn ni mwinjilisti mashuhuri. Ndugu, Ndugu Oral Roberts, mwinjilisti mwingine mashuhuri. Na—na Ndugu Tommy Hicks, na wengi sana wa hawa wainjilisti mashuhuri walioko nchini leo, unafikiri inakupasa kungojea mpaka watakapopitia hapa, ili kuponywa. Hivyo sivyo, sivyo. Mchungaji wako ana mamlaka yale yale ambayo yeyote wa hao anayo. Naam, bwana.

²⁷¹ Hakuna watu wakubwa miongoni mwetu. Kama wapo, basi mtu huyo amejiondoa mwenyewe kwenye Ushirika. “Sisi sote ni mmoja katika Kristo Yesu.” Hiyo ni kweli. Sisi ni mmoja. Hakuna watu wakubwa miongoni mwetu. Unapokuwa mkubwa, u—umekwisha kujiondoa nje, mbali na Mungu. Sivyo tulivyo.

²⁷² Na—na ikiwa mchungaji wako hayuko, jambo tu likupasalo kufanya ni kuamini Neno ambalo umemsikia akihubiri kuhusu Yesu Kristo. Hivyo tu. Mnaona? Kuna mambo makuu yanayofanywa.

²⁷³ Sasa angalieni. Hebu tutafakari juu ya maskini yule mwanamke tuliymrejea jana usiku. Wakati mmoja Yesu alikuwa akivuka bahari . . .

²⁷⁴ Laiti tungalikuwa na wakati, majuma machache hapa Tucson. Ambapo, mnaona, jambo ni kwamba, ni pagumu. Unaingia mahali, yote ni mapya kwa watu, wanaona tu jambo fulani mara moja, kasema, “Jamani, kidogo hilo ni la kigeni,

bali sijui.” Mnaona? Mimi sipo hapa muda mrefu kutosha mpate kufahamu, mpate kuliona.

²⁷⁵ Sikilizeni. Nimeona makumi elfu ya maono ambayo Bwana Mungu amenipa. Na ninajua wapo watu hapa ambao wameifuata mikutano, labda mahali pengi. Ni wangapi wamewahi kuwa katika mikutano mingine? Hebu tuone mkono wako. Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Hapajawahi kuwa na neno moja lililonenwa ila lile ambalo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli? Kama ni kweli, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakuna mtu anayeweza kusema... Kama kuna mtu yeyote anayeweza kusema walipata kuna moja ya hayo maono likikosea, uko huru kusimama na kuniambia hivyo. Ninaweza kusema hivyo kote ulimwenguni, kumi mara mamilioni ya watu.

²⁷⁶ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hawakujua kabisa Hiyo ilikuwa ni nini.

²⁷⁷ Sasa, watu kutoka maskanini, kumbukeni tu. Kuna watu wengine hapa ambao wamekuja. Ninaona wawili wa marafiki zangu hapa, Bw. na Bibi Dauch wameketi hapa, na Bibi Brown, kutoka huko Ohio. Jambo hilo la Hilo kuwa huko juu, na ile sauti iliyotokea namna hiyo, iliyorudi kwa ajili ya ile Mihuri Saba, lilitabiriwa, kila sehemu yake, majuma na majuma na majuma kabla halijatimia. Ni wangapi hapa ndani walio shahidi wa hilo, walikuwa mkutanoni na kulisikia likitajwa? Inueni mikono yenu, walio humu jengoni. Haya basi. Nayo sayansi inajitahidi sana kulichambua.

²⁷⁸ Kama wakati George J. Lacy alipoichunguza hiyo, nilimwambia. Nikasema, “Ni kama tu Nuru ya kaharabu. Inawaka kule.”

Nao wakasema, “Loo, ni saikolojia.”

²⁷⁹ Bw. Lacy akasema, “Nilifikiria ilikuwa ni saikolojia, pia, bali,” kasema, “jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia.” La. Ilikuwa pale. Ni kitu gani? Mnaona?

²⁸⁰ Sasa angalieni. Huko nyikani, wakati Mungu alipowaongoza Israeli kupitia nyikani, Yeye aliwaongoza watu kupitia nyikani kwa Kristo. Ni wangapi wanaojua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanajua ya kwamba Malaika wa agano alikuwa ile Nguzo ya Moto, alikuwa ni Yesu Kristo? [“Amina.”] Hakika, alikuwa. Hakika. Yeye alisema, aliwaambia, pale katika Yohana Mtakatifu 6.

²⁸¹ Walisema, “Hakuonekana ana umri uliozidi miaka hamsini; naye akasema, ‘Ibrahimu asijakuwako?’”

²⁸² Akasema, “Ibrahimu asijakuwako, MIMI NIKO.” Alikuwa MIMI NIKO aliyekuwa kwenye kichaka. Na Yeye akasema, “Mimi...” Yeye...

Wao wakasema, “Tulinywea maji kutoka Mwambani.”

283 Na Yeye akasema alikuwa Ndiye huo Mwamba. Amina. Mnaona, sio “Nilikuwa.” “MIMI NIKO.” Yeye alisema, “Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.”

284 Sasa, Nguzo hiyo hiyo ya Moto iliyokuwa nyikani, pamoja na wana wa Israeli, ilifanyika mwili, Mungu aliyefanyika mwili miongoni mwetu, katika umbo la kuwa Mwana wa Mungu, aliyemtia bikira uvuli na kumzaa Yeye, kusudi Mungu aweze kufanyika mwanadamu apate kufa, kulipa gharama ya sheria Yake Mwenyewe. Mnaona? Ni Injili.

285 Halafu basi akasema, sasa, “Nilitoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu.”

286 Na mara baada ya kifo Chake, kuzikwa na kufufuka, kulikuwako na maskini Myahudi mmoja aliyekuwa na hasira kali na kujaribu kumweka kila mtu gerezani. Naye alikuwa njiani mwake akienda Dameski, akiwa na amri kutoka kwa kuhani mkuu, kumshika kila mtu. Na mara yapata wakati wa adhuhuri, alipigwa akabwagwa chini barabarani. Ndipo alipoangushwa, aliangalia juu, na palikuwapo na Nuru kuu iliyoyapofusha macho yake. Ni wangapi wanajua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Nguzo ile ile ya Moto. Mnaona?

287 Ndipo akasema, “Bwana!” Akiwa Myahudi, alijua hiyo ilikuwa Nguzo ile ile ya Moto iliyokuwa nyikani. Akasema, “Bwana, U Nani Wewe?”

288 Akasema, “Sauli, Sauli, mbona waniudhi Mimi? Ni vigumu kwako kuipiga teke michokoo.”

Akasema, “Bwana, U Nani Wewe?”

289 Sasa, ngojeni. Nguzo ile ile ya Moto, Yeye alisema, “Mimi ni Yesu.” A-ha. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

290 Mnakumbuka usiku mmoja wakati Petro alipokuwa gerezani? Kitu kile kile kilikuja gerezani, kikaifungua milango mbele yake, na kumtoa nje.

291 Ni kitu gani? Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele. Sasa, kama hicho hakikuwa, kama hicho kilikuwa kitu kingine, kingefanya kazi ya aina nyingine. Bali kama hicho ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa nyikani pamoja na Israeli, na pia alikuwa ndani ya Yesu Kristo, Sasa yuko Kanisani. Anafanya kazi zile zile kwa kuwa ni Nuru ile ile. Mnaona? Ni Roho yule yule. Laiti ungaliweza tu kuamini hilo, rafiki! Sio mimi; Yeye! Mnaona? Yeye ndiye Kuhani Mkuu.

292 Maskini mwanamke mmoja, siku moja, aliamini ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Alikuwa na kutokwa na damu. Basi akasema moyoni mwake, “Laiti ningaliweza tu kugusa mavazi Yake!”

²⁹³ Nafikiri alipata hilo kutoka, bila shaka, Eliya, na “kuitwaa ile fimbo.” Na hapo ndipo nafikiri Paulo alitoa, “kuwekea lesa,” na kadhalika, ilikuwa ni kile mtu mwingine alikuwa amefanya.

²⁹⁴ Naye akasema, “Kama ninaweza tu kugusa vazi Lake, ninaamini nitapata afya.” Ndipo akajisukumiza kwenye umati mpaka akaligusa vazi Lake. Sasa, vazi la Kipalestina hupwaya, nalo lilikuwa na vazi la ndani. Na kwa hiyo alienda akaketi chini.

²⁹⁵ Kimwili, Yeye asingeweza kuuhisi, mnaona, kwa sababu vazi hilo ni joho linalopwaya. Lakini, Yeye akasimama.

²⁹⁶ Na kila mtu alikuwa akimkumbatia, “Aloo, Rabi! Nabii wa Israeli, tunafurahi kuwa na Wewe hapa pamoja nasi,” na kadhalika.

Yesu akasimama, akasema, “Ngoja kidogo. Ni nani aliyenigusa?”

²⁹⁷ “Mbona,” Petro akasema, “Bwana!” Akamkemea. Kwa maneno mengine, kasema kitu kama, “Bwana, usiseme chochote kama hicho. Watu watakuwa wanakushangaa Wewe. Ati ni nani ‘aliyekugusa’ Wewe? Kila mtu wamekukumbatia. Kila mtu anakupapasa. Usiseme, ‘Ni nani aliyenigusa?’”

²⁹⁸ Akasema, “Lakini huu ni mguso tofauti. Unaona? Naona kwamba nguvu zimenitoka.”

²⁹⁹ Akaangalia kwenye umati huo. Naye maskini mwanamke huyo huenda alikuwa amesimama. Huenda ameketi. Ama, popote alipokuwa, kulikuwa na jambo lililokuwa limetendeka. Na Yeye akamwona. Asingeweza kujificha. Mnaona? Alikuwa amemgusa Mungu, kupitia Mtu huyo. Nguvu, uweza, ulikuwa umemtoka. Akamwambia kuhusu damu yake, kutokwa na damu, nako kulikuwa kumekoma.

³⁰⁰ Sasa, Yesu huyo huyo ndiye Kuhani Mkuu yule yule leo. Biblia ilisema hivyo. Hiyo ni kweli, ndugu wahudumu? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Kwamba “Yeye sasa ni Kuhani Mkuu, anayeketi mkono wa kuume wa Mungu, Baba. Ameketi pale, akiishi daima kufanya maombezi, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.”

³⁰¹ Sasa, huna kadi ya maombi. Hutakuwa hapa juu mstarini. Lakini kama unataka kujua kama ni kweli ama si kweli, wewe mwambie tu Mungu usiku wa leo, “Baba wa Mbinguni, mimi ni mgonjwa. Sina budi kupata usaidizi. Na ni—ninatumia imani yote niliyo nayo. Ninajua si yule mtu anayesimama pale. Huyo ni mwanamume tu kama nilivyo mimi, ama mume wangu, ama ndugu yangu. Mnaona? Bali ninaamini mtu huyo alisema Kweli, kwa sababu ni Maandiko. Pia ninaamini ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu sasa. Jambo hilo, jalia nikuguse Wewe, Bwana, na Wewe uwe yeye yule jana. Wewe. . . Huyo ndugu hanihui mimi. Lakini Wewe zungukia nyuma ukaitumie midomo yake, na unene nami na kusema kama ulivyosema na mwanamke yule.”

³⁰² Ninawapa changamoto, katika Jina la Yesu Kristo, mwe na imani kama hiyo, na mwone litakalotukia. Mwone kama ni kweli au sivyo. Ni kweli. Aminini tu. Na kama mnaweza kufanya hivyo, vema, Mungu atawabariki.

³⁰³ Sasa, je! kuna mtu yeyote hapa ambaye hajawahi kuwa kwenye mmoja wa mikutano hapo kabla? Inua mkono wako. Jamani! Loo! Tuna furaha kuwa nanyi hapa usiku wa leo. Mungu awabariki. Mkutano mdogo tu, wakati wa ushirika. Na ndio kwanza nikimbie humu, na wasiwasi, kwa siku mbili au tatu usiku, kisha niondoke. Labda wakati mwingine, Mungu akipenda, wahudumu wakipenda, tungeweza kurudi hapa wakati mwingine, tuwe na mkutano mzuri, ambamo tunakaa majuma mawili ama matatu.

³⁰⁴ Na watu wagonjwa, wakati mwingine, watakuwa na, kitu kama, ki—kivimbe ndani yao. Hata hawajui kivimbe hicho ni nini. Sasa, ni uhai, kama ugonjwa wa kuua, ama chochote kile. Ni uhai. Ni uhai ambao hauninii. . .

³⁰⁵ Tuseme, mkononi mwangu, hamna kansa hapo sasa. Labda itakuwako, siku moja. Kwa kawaida, kansa, inatokana na. . . Ni seli mwitu.

³⁰⁶ Na kama vile baadhi yenu ninyi akina dada mkipitia wakati wa kukata hedhi, nao wanawandunga sindano hii ya homoni. Kamwe usifanye hivyo. Wewe mtumainie tu Mungu. Homoni ni seli mwitu, nawe unaweza tu kansa moja kwa moja ndani yako. Unaona? Mimi si. . . Daktari, usifikiri ninajaribu kupachukua mahali pako hapa. Lakini nimekwisha kukutana nayo kwa wingi sana katika mstari wa maombi. Mnaona? Kwa hiyo, jambo la kufanya, weka tu imani yako kwa Mungu. Naye daktari wako mzuri, mwaminifu, daktari wako nyumbani, atakwambia hiyo ni kweli. Wewe mwamini tu Mungu na umtumainie. Atakupitisha kwenye vivuli hivyo. Sikuzote Yeye yuko hapo kukusaidia. Hiyo ni kweli.

³⁰⁷ Angalieni. Tunaona, vipi kama kivimbe hicho, kikianza kukua? Ni kitu gani? Ni uzidishaji wa seli, seli moja ikilundikana juu ya nyingine.

³⁰⁸ Hivyo ndivyo ulivyo wewe, pia, uzidishaji wa seli. Vema, unajua ulikotokea. Ndoa takatifu kati ya baba na mama, seli moja ndogo sana. Kama nilikuwa niurarue mwili wako wote, usiku wa leo, nichukue seli baada ya seli, ingefikia kwenye huo uhai mmoja mdogo. Ndani ya uhai huo, hakika, kuna kemia ya damu, na ndani ya damu hiyo kuna uhai, na uhai huo ndio wewe. Sasa, ikaanza kuongeza seli.

³⁰⁹ Na kwa hiyo, kila kitu kwa jinsi yake, ndege kwa ndege, mbwa kwa mbwa, mwanadamu kwa mwanadamu. Na inafanya. . .

³¹⁰ Lakini, unaona, ibilisi hana umbo. Kansa, inaitwa kansa, inatokea neno “kaa,” ambalo linamaanisha “miguu iliyotanda

kote,” inaanza kunyonya. Inanyonya damu yako kutoka kwako. Ni uhai mwingine. Ni uhai unaoishi ndani yako. Kwa hiyo, kuna uhai wa mwanadamu. Na kuna uhai mwingine; na huo ndio ninaozungumzia, ni uhai huo. Sasa wanaposema, sasa, mnaiita, daktari anaiita, “kansa,” na baadhi yao wanaiita mtoto wa jicho, na baadhi yenu mnaiita vitu mbalimbali, majina ya tiba. Lakini, Yesu aliita “ibilisi,” na hivyo ndivyo ilivyo. *Ibilisi* maana yake ni “mtesi,” naye yuko hapo kuuchukua uhai wako.

³¹¹ Sasa, wakati mwingine, daktari anaweza kukata hapo na kuitoa yote. Hilo ni zuri sana. Lakini vipi kama imeshikilia sana hivi kwamba, haiwezi kutoka? Sasa, hatujishughulishi na uvimbe huo, wenyewe. Tunashughulika na uhai ulioko ndani ya uvimbe huo, sasa, wakati unaposema, “Shetani, toka.”

³¹² Nami ninaweza kukuthibitishia. Acha mtu aweke mikono yao mkononi mwangu, na kukuthibitishia, kuonyesha ma—matokeo inayosababisha. Mmeliona likifanywa, wengi wenu. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³¹³ Angalieni sasa. Kama uhai huo ukitoka hapo, kunafanyika nini? Unarudi kesho yake, linasinyaa. Kitu chochote kinajua, baada ya chochote... Mtu yeyote anajua, kitu chochote kinapokufa, kinasinyaa. Ukimwua kulungu, kisha umpime na kuwaambia ndugu ana ratili ngapi, kisha umrudishe kwenye ratili asubuhi, atakuwa mwepesi pauni kadhaa. Mtu anapokufa, aliye na meno bandia, wanayatoa; jicho bandia. Maana, wataninii... hayo, yanasinyaa. Yatatoka.

³¹⁴ Vema, basi, akiisha kukaa hapo muda mrefu sana, kama mnyama mdogo, mbwa, akikanyagwa barabarani, akikaa kwenye jua, huanza kuvimba, kisha anakuwa mkubwa kuliko alivyokuwa mara ya kwanza. Mgonjwa basi ataanza kuwa mgonjwa baada ya yapata saa sabini na mbili, wakati uharibifu unapoingia. Wataanza kusema, “Loo, ninaumwa kuliko nilivyokuwa. Nimepoteza uponyaji wangu.”

³¹⁵ “Na wakati roho mchafu anapomtoka mtu, hutanga-tanga mahali pasipo na maji, anarudi tena.” Mnaona? Basi kama kweli huamini, haijalishi ataondolewa mara ngapi kutoka kwako, kama hujui jinsi ya kulikubali na kuliadini! Anaporudi, ungali unajua ameondoka; na kama ukimkubali, basi hakuna kitu ila mauti. Lakini kuna shida gani? Unaweka ninii... .

Vipi kama ulikuwa na nyoka ndani yako, mrefu *hivi?* Ungekufa.

³¹⁶ Vema, ni kitu gani? Moyo wako unapiga na kuusafisha mkondo wa damu. Na hiyo ndiyo inayosababisha homa, ni ambukizo. Halafu basi wakati kivimbe hicho, kinachokaa katika mwili wa mwanadamu, na kimekufa, basi ambukizo linaingia, ama kinaanza kuvimba, nao moyo hauna budi kuupiga huo utoke, kuisafisha damu. Mbona, bila shaka, hali yako inakuwa mbaya zaidi.

³¹⁷ Lakini watu, hapo, wasio na imani, wanaingia tu mbio, na kweli wanapata nafuu. Ninaona watu. . .

³¹⁸ Usiku mmoja, mtu mwenye watoto wa macho juu ya macho yake, alishuka akaenda na kucheza piano, na angeweza kuona. Alikuwa huku na kuichukua Biblia ii hii na kuisoma. Na yapata siku nne usiku baadaye, hata asingeweza kuuona mkono wake mbele zake. Akarudi, kasema, “Nilipoteza uponyaji wangu.” Lilikuwa tu ni jambo jema kuwa pale. Alikuwa.

³¹⁹ Nikasema, “Ndugu, hilo ni kosa. Wewe—wewe, umefanya. . . Ulishuku.”

Akasema, “Vema, Ndugu Branham, niliponywa. Lakini. . .”

³²⁰ Nikasema, “La, ni mtoto wa jicho akivimba, bwana. Endelea tu kuamini. Usitie shaka. Ukitia shaka, itarudi. Wewe endelea tu kuamini. Ulisema uliamini. Halafu, unaghairi yale uliyosema. Usiseme hivyo ‘sipokuwa unaliamini.’” Nikamtia moyo na kumwambia. Akakaa kule, alikuwa kule majuma mawili. Mwishoni mwa hayo majuma mawili, angeweza kusoma Biblia vizuri kama mtu yeyote mwingine alivyoweza. Mnaona?

³²¹ Sasa, kama hakuwa amekuwa na maagizo juu ya jambo la kufanya, na hilo ndilo unalopata, kuingia mbio namna hii. Basi muda si muda mwajua, basi yote yanamwangukia mchungaji, nao wanasema, “Vema, hawakuponywa.” Mnaona, ni kwa sababu kusanyiko halijafundishwa. Hawaelewi jinsi ya kufanya, kile kiwapasacho kufanya. Nao kwa jumla, hawana, imani. Wana matumaini mengi sana.

³²² Lakini, sasa, kile ninachotaribu kufanya, sio kwenu kusema, “Unajua nini? Ndugu Branham aliniwekea mikono, na, ndugu, nilipona.” Sitaki hata kuwagusa. Nawatakeni mumguse Yeye. Mnaona? Sina uhusiano wowote nalo.

³²³ Lakini katika karama ambayo Mungu amenipa, kama ninaweza kumdhahirisha Kristo, kumwonyesha na kumleta kwenye uhalisi hapa mbele zenu, Neno Lenyewe lililofanyika mwili miongoni mwetu, na kuonyesha ya kwamba ni Mungu, basi wewe mguse tu Yeye na uone linalotukia. Mnaona ninalomaanisha, enyi marafiki?

³²⁴ Hutaki kitu fulani kikubwa. Ukitaka, huwezi kuenda sehemu ndogondogo. Nilikuwa hudumani, miaka kadhaa iliyopita. Sijawahi kuiruhusu mikutano yangu kupanuka kufikia mahali. Sina televisheni zozote. Sina chochote ninachouza. Si—sina chochote, Kristo tu. Na mimi. . . Kama wengine. . . Mimi huenda kwenye sehemu hizo ndogo sana ambako baadhi ya hao ndugu walio na pogramu hizi kubwakubwa wasingeweza kwenda, kwa sababu inawabidi kuwa na maelfu ya dola kila siku, kudumisha programu yao. Hainibidi kuwa na chochote, ni kuwa tu na Mungu zaidi. Mnaona? Nami ninaweza kwenda kokote anakonituma Yeye. Mnaona? Na huko ndiko ninakoweza kwenda.

325 Nilihubiri uamsho hapa si muda mrefu uliopita, katika kanisa lililokaa watu ishirini. Ilikuwa ni la kusikitisha, bali tuliufanya, kwa vyovyote vile, kwa sababu Bwana aliniambia niende huko. Mnaona? Kisha ninaenda na kuihubiria halaiki ya watu laki tano. Mtu fulani anaufadhili na kunipeleka kule. Sihofii lolote. Ninahofia tu kujiweka sawa, mbele Zake. Mnaona? Yeye hunituma kokote anakotaka kunituma.

326 Sasa, usiku wa leo, kama nijuavyo mimi, katika mstari huu, watu ni wageni kwangu.

327 Ni wangapi walioko huko nje, walio wageni kwangu? Inua wako... Unayejua sijui lolote kukuhusu, inua mkono wako, u— unamhitaji Kristo. Vema. Aminini tu sasa. Nafikiri ilikuwa asilimia mia moja.

328 Sasa, wakati mstari huu wa maombi ukiendelea hapa juu, wewe anza kuomba huko chini, ili Mungu atimize. Na kama atafanya hivyo, utaamini, sivyo? Semeni “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

329 Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba hivyo ndivyo hasa Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe kama Masihi wa Mungu? Ni wangapi wanaojua hilo, kutoka kwake? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mnaona? Ni hakika. Ni hakika. Na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. “Sifanyi lolote mpaka nilione, yale nimwonayo Baba akifanya.”

330 Ninataka kuchukua kila roho humu ndani chini ya mamlaka yangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

331 Endeleeni kuketi. Ketini kimya. Msiende huku na huku. Mnapotembea, unaona, kila mmoja ni roho. Mnajua hilo? Kama sivyo, ungekuwa umekufa. Mnaona? Na—na kutokuamini kwako... Na mimi nikisema, “Inamisha kichwa chako,” kiinamishe. Nikisema, kama akikuita usimame, simama. Na lolote asemalo fanya, fanya tu Hayo. Kwa sababu, sio mimi. Ni Yeye.

Sasa anzeni mstari wenu wa maombi, popote pale.

332 Baba wa Mbinguni, haitachukua muda mrefu, mpaka wakati utakapokwisha. Wakisimama hapa nyuma yangu usiku wa leo ni wachungaji, wahudumu, ambao wametabiri na kudai ya kwamba saa itakuja wakati hili litatendeka. Maskini mashujaa fulani, miaka mingi iliyopita, wakisimama pembeni, wameshika gita mkononi mwao, wakidai kwamba itakuja siku. Basi hawa hapa baadhi yao hapa usiku wa leo, na wana wao wapo hapa. Baba, walitengeneza tu njia kuifanya halisi. Sasa jalia tuipokee, Bwana. Tujalie. Pia jalia, pamoja, tushiriki kwenye karama hii kuu ambayo Mungu ametutumia, Yesu Kristo. Tujalie, Baba.

333 Sasa, Bwana, Wewe unajua ya kwamba sijui mmoja wa hawa watu. Sijui chochote kuwahusu. Wewe unawajua wote.

Nami ninajaribu kuwafanya watu waone, Bwana, ya kwamba si watu wakuu, kanisa kuu. Ni Mungu mkuu, na Yesu Kristo. Naomba ya kwamba utajalia ajulikane kwetu usiku wa leo, kwa unyenyekevu.

³³⁴ Sasa nimelipa kusanyiko changamoto, Bwana, kukutazama Wewe. Basi jalia baadhi yao huko nje, Bwana, mtu fulani, ninaomba ya kwamba Wewe utamjalia Roho Mtakatifu achunguze imani fulani hapo usiku wa leo, ambayo italifanya kusanyiko kuchochewa, kuona kwamba kuna kitu kinachoendelea. Basi jalia wafahamu, na kila mmoja aponywe. Jalia kusiweko na mtu mgonjwa miongoni mwetu, usiku wa leo, hapo ibada itakapomalizika. Jalia kila mtu asiyeokoka aokolewe, wakati wanapojisikia na kujua kwamba wako katika Uwepo wa Mungu yule hasa atakayewahukumu Siku moja. Tunayakabidhi yote Kwako sasa. Pia ninajikabidhi mwenyewe Kwako. Nitumie, Bwana, vile unavyoona inafaa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

³³⁵ Sasa, na—nawaomba mwe watulivu kabisa na katika maombi. Sasa, wazieni tu... Sasa, kama mtu yeyote hafikiri kwamba hili linatoka kwa Mungu, basi, katika Jina la Yesu Kristo, nakupa changamoto uje hapa ukafanye jambo lile lile. Halafu basi, kama huwezi, usiseme chochote juu yake. Yatafuteni katika Maandiko, mnaona. Mnaona?

³³⁶ Sasa, kadiri nijuavyo mimi, pamoja na Biblia ya Mungu hapa mbele zangu, na kundi hili la watu walioketi hapa, wakiniangalia, na mbele ya watu hawa, mwanamke huyu ni mgeni kwangu. Simjui. Yeye ni mwanamke tu anayesimama hapo. Sijui lolote kumhusu.

³³⁷ Kama ni mgonjwa, nami—nami nilikuwa na njia yoyote ya kumponya, hakika ningemponya. Unaamini hilo, sivyo? Ningemponya kama ningaliweza. Lakini, siwezi. Hakuna yeyote mwingine anayeweza.

³³⁸ Uponyaji hutoka kwa Mungu, na Yeye tayari amewaponya. Lakini kama—kama Mungu angeweza kufanya jambo fulani, kukufanya ufahamu ya kwamba Yeye angali hapa, na Yeye hapa kuitimiza ahadi Yake. Kama Yeye hutimiza ahadi *hii*, basi ataitimiza, Yeye hutimiza ahadi ya uponyaji, hakika. Mnaona?

³³⁹ Halafu basi kama—kama Yesu alikuwa amesimama hapo usiku wa leo, amevaa suti hii aliyonipa, nawe ungemwendea na kusema, “Bwana, wangu, mimi ni mgonjwa. Ninaomba Wewe uniponye.”

³⁴⁰ Ninaamini lingekuwa jambo kama hili. Yeye angesema, “Mtoto wangu, hivi huamini Maandiko matakatifu? Nilikufa kwa kusudi hilo. Nilinunua uponyaji wako pale Kalvari, nilipoteseka kwa ajili yako.”

“Lakini ninajua Nani kwamba Wewe ni Nani? Wewe ni Bwana wangu?”

341 “Vema, nilifanya nini nilipokuwa hapa duniani, hapo awali, kujitambulisha Mwenyewe kwa watu, kwa Wayahudi na Wasamaria pia?”

342 Hata wakati mmoja mwujiza huo haukufanywa mbele ya Mmataifa, maana Mataifa hawakuwa wakiutarajia. Sasa ndiyo siku ya Mataifa, wakati wanapopata yao sasa. Na hii ndiyo siku, ambayo Yeye alisema, “Neno dhidi ya Roho Mtakatifu, akiitwa pepo mwovu, halitasamehewa watu.”

343 Sasa, mwanamke huyu, sote wawili hapa mbele za Mungu, na chini ya Biblia, sisi kabisa, mnaona, hatufahamiani, kamwe hatujawahi kuonana mmoja na mwingine. Wala sijui, sina fununu hata moja, sababu ya yeye kusimama hapo. Sijawahi kumwona maishani mwangu, na hii ni Biblia mikononi mwangu. Na kama mhudumu, ingefaa nini kwangu kusema hivyo, wakati ni makosa, kujihukumu mwenyewe?

344 Si lazima niwe hapa nikifanya hili. Nimekuja kwa sababu ninajisikia niko katika mapenzi ya Mungu. Nimekuja kwa sababu kwamba ninajua ya kwamba Siku ya Hukumu itaipiga Tucson siku moja. Naye Mungu anajaribu kuwapelekeeni Ujumbe, na mimi sina budi kuwa shahidi Wake. Hakuna chochote kwangu, mimi ndiye mdogo kuliko wote miongoni mwenu. Mimi ni ndugu yenu tu. Ni Yesu Kristo, bali inampasa Yeye kuwa na mtu fulani kutenda kazi kupitia. Ndiye anayefanya uchaguzi huo, Mwenyewe. Alikusudia hilo tangu zamani kuwa hivyo.

345 Sasa, kama Roho Mtakatifu ataniambia kile alicheo mwanamke huyo, ama kile ambacho amefanya, ama kile, jambo fulani kumhusu, anajua, yeye atajua kama ni kweli ama si kweli. Sivyoy? Hakika. Ungejua kama ni kweli. Na kama si kweli, basi si Mungu. Bali kama ni kweli, basi ni Mungu.

346 Ni wangapi wenu wataamini sasa kwa moyo wenu wote na kulikubali? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

347 Sasa sisi hapa, chini ya kiapo, chini ya Biblia, mbele ya mashahidi Wake, mbele ya mashahidi hapa. Nayo Biblia ikiwa hapa, iliyoahidi ya kwamba mambo yaliyofanywa kabla tu Sodoma haijateketezwa yatafanywa mbele ya Mataifa, kabla ya . . .hawajaangamizwa. Wito wa mwisho kwa uzao wa Ibrahimu, uzao wa kifalme!

348 Sasa, mtu yeyote anajua, mwanamke huyu amesimama huku amefunga macho yake, akilirudia tu Neno, la maombi. Yeye ni Mkristo, kwa sababu, wakati alipokuja huku kwanza.

349 Unaona, mara moja moja, mwigaji huingia kisiri, na kujaribu kutenda kama Mkristo. Ni wangapi wamewahi kuona hilo likitukia? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mmeona kinachowapata pia. Ama wanaanguka papo hapo, ama wanapooza. Wanawabeba kuwapeleka nje, na ni hilo

tu. Hatuigizi kanisa. Mnakumbuka Phoenix, miaka michache iliyopita, juu ya hilo.

³⁵⁰ Sasa, mama huyu, kwa kweli, amelemewa na jambo fulani. Sasa, kama mngeweza kuona, kati yake na mimi, ipo Nuru. Anaanza kutoweka. Lakini inaonekana kana kwamba roho yake inasumbuka. Ana matatizo ya kiroho anayohofia. Hiyo ni kweli. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako.

³⁵¹ Kwa kubadilikabadilika, kila wakati, ninahisi hilo likija, “Yeye anasoma nia ya mwanamke huyo.” Siisomi. Nitapata huyo moja ya siku hizi, nami nitamwita, pia.

³⁵² Hebu kidogo, tutaona kama sisi, tutaona kama tunabahatisha juu ya hili. Sijui yale ilisema, kwanza. Kulikuwa na kitu fulani. Ilionekana kana kwamba kilikuwa ni matatizo ama kitu fulani. Loo, hiki hapa. Ninaona sasa. Ni tatizo la kiroho.

³⁵³ Jambo lingine, una vipindi vya magonjwa. Una ugonjwa wa ugumu unaota kwenye nyongo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? A-ha. [Dada huyo anasema, “Unakuja kwa hatua.”—Mh.] Naam, bwana. Kwa namna fulani mtu mwenye nguvu. Angalia, jambo lingine, una mzigo kuhusu mtu mwingine. Hao ni watoto fulani. Ni watoto wako, wokovu wao. Hiyo ni kweli. Ni kuhusu mtu fulani, pia, aliye hapa. Ninaweza kulihisi. Ni mume wako, na ni wokovu wake. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli. Yupu ameketi hapa sasa. [“Hiyo ni kweli.”] Hum!

³⁵⁴ Hutoki hapa. Ninakuona ukitembea mahali fulani ambapo pana vilima virefu vya kijani kibichi na maji mengi. [Dada huyo anasema, “Yesu!”—Mh.] Ni—ni mbali na hapa. Ni kaskazini kutoka hapa. Umetoka kwenye jimbo la Oregon. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli. Umetoka mahali fulani karibu na Grants Pass, ama mahali fulani karibu na hapo vilipo hivyo vilima. Jina lako la kwanza ni Lena. [“Hiyo ni kweli.”] Jina lako la mwisho ni Stovell. [“Hiyo ni kweli.”] Hiyo ni kweli. Yesu Kristo ameliheshimu ombi lako usiku wa leo. Nenda nyumbani. Mume wako amekoka; watoto wako, pia; nawe umepokea uponyaji wako. Jina la Bwana Yesu Kristo libarikiwe!

³⁵⁵ Chochote kilichokuwa, sijui. Itabidi tu kuwa kwenye kanda. Bali ninajua ilikuwa ni mwanamke aliyekuwa na imani, aliyeamini.

³⁵⁶ Mnamwamini Yeye sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele? [“Amina.”] Unajua huyo hana budi kuwa ni Roho. Sasa inategemea kile unachofikiria Hicho kilikuwa.

³⁵⁷ U hali gani, mama? [Dada huyo anasema, “Njema.”—Mh.] Sasa, hatufahamiani. Si—sikujuu. Nawe ni mdogo wa umri sana kuliko nilivyo mimi. Lakini unaamini Yesu anaweza kuniambia kilicho shida yako, ama jambo fulani kukuhusu? Ingekupa imani kuamini? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unajua

nisingejua. Ingekuwa haiwezekani kwangu kujua. Ingebidi iwe inatoka Kwake, Roho. Nawe unajua kwenye wakati huu kwamba kuna kitu kinachoendelea. Ni Uwepo Wake.

³⁵⁸ Hasa husimami kwa ajili yako mwenyewe. Una matatizo mengi sana. Una la kiroho, matatizo mengi ya kiroho ambayo yanakusumbua. [Dada huyo anasema, “Ndiyo.”—Mh.] Kwamba utaninii. . . Utapata jibu lake. Na kukufanya tu ujue ya kwamba ninajua kile ninachozungumzia, baadhi yake ni kuhusu jambo fulani linaloendelea kanisani mwenu. [“Hiyo ni kweli.”] A-ha. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Ni shughuli ya biashara. Inaendelea kanisani mwenu, ambayo hufikiri inaenda vizuri. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli.

³⁵⁹ Na jambo lingine, ninamwona mtu fulani akitokea, ambaye karibu amekufa. Ni ugonjwa wa kansa. Unaomba kwa ajili ya kansa, mtu fulani nchini mwenu. Nawe pia umetoka Oregon, kwa sababu ni nchi ile ile yule mama aliyekuwa hapa awali. Hiyo ni kweli. Pokea ulichoomba. [Dada huyo anasema, “Asante, Bwana.”—Mh.] Rudi nyumbani. Imani yako inakujalia hilo.

³⁶⁰ Kamwe sikumgusa mwanamke huyo. Lakini Mungu alimgusa, kwa ajili yake. Amini tu.

³⁶¹ U hali gani, mama. Hatufahamiani mmoja na mwenzake. Bwana Yesu anatuajua sote wawili.

³⁶² Sasa, hebu kidogo. Jambo fulani lilitukia kwenye kusanyiko. Iweni na kicho kabisa. Kulikuwako na mwanamume aliyetokea, mbele ya mwanamke huyu hapa, mtu mwenye imani. Endelea tu kuomba, yeyote yule. Nililikosa. Endelea tu kuomba.

³⁶³ Tena, unaona, kuzungumza na wewe. Kila mtu ana roho. Mnaona? Nao watu wanaanza kuamini, mnaona. Na inalifanya, mnaona, imani ya kila mtu ikivuta kwa kila njia, mnaona. Hiyo ndiyo sababu inanibidi kumleta mtu fulani hapa mbele yangu tu.

³⁶⁴ Kuna hata wahudumu wanaoketi hapa, walio wagonjwa, wanaoomba sasa hivi. Mnaona? Na hiyo ni. . . Mnaona?

³⁶⁵ Nami nimewaita, nyinyi mlio na kadi ya maombi. Sikujui, bali Mungu anakujua. Basi kama Bwana Yesu ataniambia jambo fulani maishani mwako ambalo umefanya, ulilopaswa kufanya, ama shida fulani uliyo nayo, kama wewe ni mgonjwa, huenda ikawa ni tatizo la kinyumbani, ama huenda ikawa ni tatizo la kifedha. Sijui ni nini. Lakini chochote kilicho, utajua kama ni kweli ama si kweli, kama Yeye akilitaja. U—utaamini, na kuamini ya kwamba—ya kwamba wewe sasa uko katika Uwepo Wake? Si uwepo wangu, au hawa watu, waliopo, hiyo haingekufanya kujisikia jinsi unavyojisikia sasa. Ni Uwepo Wake.

³⁶⁶ Kuna mtu anayeendelea kusimama karibu na mwanamke huyu. Ni mtu mnene. Ni kitu fulani. Ninaliona. Wewe ni rafiki

ya mtu ninayemjua, Paul Cain, mhudumu. Unamjua. Hiyo ni kweli, maana yule pale. Ni. . . Hiyo ni kweli. Amekuombea, mtu huyu. Na tatizo lako, una henia, na hiyo henia iko kwenye kiwambo. Hiyo ni kweli. Na imesababisha matatizo na kila namna ya maradhi. Hutoki hapa. Umetoka. . . Uko magharibi mwa hapa. Umetoka California. Unamwamini Yesu Kristo? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Utamkubali? Binti Moss, unataka kurudi nyumbani na kupata afya? Rudi na uamini. Mwamini Mungu sasa. Usitie shaka, nalo litatimia.

³⁶⁷ Mnamwamini Bwana Yesu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

³⁶⁸ U hali gani? Hatufahamiani, mmoja kwa mwingine, nadhani. Bwana Yesu anatumjua sote wawili. Sikujui, bali Bwana Yesu anakujua.

³⁶⁹ Hiyo ni—Hiyo ni Nuru, nayo Hiyo inaendelea tu kuondoka jukwaani. Nyinyi nyote endeleeni kuamini namna hiyo. Endeleeni tu, endeleeni tu kuamini. Mnaona? Endeleeni kuomba. Sawa.

³⁷⁰ Unasumbuliwa na kivimbe. Unaamini kwamba Bwana Yesu anaweza kuniambia mahali kivimbe hicho kilipo? Kiko kwenye titi lako la kulia, pafu. Hiyo ni kweli. Hutoki hapa. Kuna mtu aliyekutuma hapa. Aisee, umekuwa kwenye mstari wa maombi hapo awali. Hiyo ilikuwa ni. . . Umetoka Chicago. Na uliponywa wakati mmoja mkutanoni, ambapo uliambiwa, kwa kuweko na tatizo ubavuni mwako, ama mguu, au kitu kama hicho. Na wewe uliponywa katika mkutano huo. Pia mtu mwenye mvi, naye ana mvi kwenye masha-. . . Ni Mchungaji Matsson-Boze, ambaye alikuwa mchungaji wako huko kwenye kanisa la Philadelphia, huko ndiko umetoka, alikutuma hapa usiku wa leo. Hiyo ni kweli. Yesu Kristo anakufanya mzima. Rudi Chicago, ukishangilia. Yesu Kristo anakufanya mzima.

“Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.”

³⁷¹ U hali gani? Hatufahamiani mmoja na mwenzake. Sikujui wewe, bali Yesu Kristo anakujua. Unaamini ya kwamba Yeye anaweza kunipa Roho Wake? Ambapo, mimi sitoshelezi kama mhudumu, unajua, kuwa, unajua. Bali—bali kwa karama katika Biblia, ambayo imeahidiwa katika siku za mwisho, “kuirudisha Imani ya watoto iwarudie baba zao.” Unaamini saa imewadia kwa ajili ya jambo hilo, na kwamba huduma hiyo inafanya kazi Kanisani leo hii?

³⁷² Wewe, pia, umetoka Chicago, maana ninakuona ukitembea barabarani. Inaonekana kana kwamba ni Barabara ya Clark, kwangu mimi. Hiyo ni kweli. Nawe unaugua yabisi kavu, mateso mbalimbali mwilini mwako. Unaweza kurudi sasa. Imani yako inakuponya. Mungu akubariki. Nenda, ukiamini kwa moyo wako wote.

373 Unaamini Mungu huponya yabisi kavu? Basi rudi kwenye kiti chako na umshukuru Yeye kwa ajili yake. Ponywa. Pata afya.

374 Unaweza kuja mbele, mama? Ungetaka kwenda ukale na kujisikia vema tena, maskini tatizo hilo la tumbo liondoke? Nenda, ukale. Yesu Kristo akuponya.

375 Mama, yule mama pale aliye na huyo mtoto, unaamini Mungu atamponya mtoto huyo? Ninaweza kukwambia tatizo la mtoto huyo, bali siwezi kumponya. Angalia hapa, kipenzi. Nina msichana mdogo huko nje, karibu tu kama wewe. Ninamwacha mara nyingi, akilia, kama unavyofanya sasa, nipate kwenda kuwaona wasichana wadogo. Unaamini Yesu anaweza kuponya tatizo la moyo na kukufanya mzima? Njoo hapa. Njoo kwangu.

376 Baba wa Mbinguni, hebu nguvu za Roho Mtakatifu aliyepo sasa, ayaokoe maisha ya mtoto huyu. Katika Jina la Yesu Kristo, ninayaombea maisha yake. Amina.

Usilitilie shaka. Usilitilie shaka, dada. Nenda, amini, na itakuwa sawa.

Amini sasa kwa moyo wako wote.

377 Njoo, mama. Unaamini Mungu anaweza kuponya tatizo hilo la kina mama, tatizo la kike, kutokwa na damu kutakoma? [Dada huyo anasema, “Ndiyo, bwana.”—Mh.] Rudi. Liamini kwa moyo wako wote, na upone. Unaona? Unaona?

378 Ungetaka kupumua tena, vizuri na huru, na kuondokewa na maskini pumu hiyo na kadhalika? Nenda nyumbani na uliamini kwa moyo wako wote. Unaweza kuponywa na kufanywa mzima. Amini kwa moyo wako wote.

379 Mungu huponya tatizo la moyo, pia. Hiyo ni kweli. Unaamini hilo? Rudi tu na kusema, “Asante, Bwana Yesu.” Na ulisifu Jina Lake, nawe utakuwa mzima.

Katika Jina la Yesu Kristo, mjalie hili.

380 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni wangapi wanaamini? [“Amina.”]

381 Vipi kukuhusu wewe hapo kwenye hayo machela? Unaamini? Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, na—namaanisha, mtumishi Wake? Hilo huwakwaza watu. Sikujui. Wewe ni mwanamke tu aliyelala hapo. Ninaona uko kwenye machela. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Kama Mungu anaweza kunifunulia kilicho shida yako, utamkubali Yeye kama Mponya wako? Umetiwa uvuli wa mauti. Kuna kivuli cheusi juu yako. Kama ukikaa hapo, utakufa. Haifai kitu kwenda kwa daktari; yote yamekwisha, kama ajuavyo yeye. Ugonjwa unaokuua ni kansa. Kwa nini usimkubali Yesu Kristo kama Mponya wako? Inuka kutoka kwenye machela yako, uyachukue na uende nyumbani, ukapate afya. Utaamini hilo? Likubali, na uende nyumbani basi. Simama, na uamini. Naye akasimama.

³⁸² Vipi kukuhusu wewe uliyeinua mkono wako juu hapo, uliyevaa hilo koti jeupe? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, bwana? Una namna fulani ya vipindi. Ni kifafa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono huo mwingine. Sasa mwamini Yeye, kwa moyo wako wote, na hutakuwa na kipindi kingine. Ninakupa changamoto kuliadini.

³⁸³ Mwanaume huyu aliyeketi hapa akiniangalia, akiwa na shati. . . akiangalia moja kwa moja hapa juu. Unaugua ugonjwa wa moyo. Sikujui mimi, lakini hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Hebu nikwambie tena. Wewe ni mhudumu. Una makanisa unayoyatembelea. Inaonekana kana kwamba ni jamii ya watu weusi. Ni Mexico. Hiyo ni kweli. Unamjali sana mtu fulani. Huyu ni mke anayeketi hapo karibu nawe. Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Siwezi kumponya, lakini kama ninaweza kukwambia shida yake, utaamini kwa ajili ya uponyaji wake? Yeye ni kiziwi masikioni mwake. Weka mikono yako juu ya masikio yake, na uamini kwa moyo wako wote, naye anaweza kuponywa.

³⁸⁴ Ni wangapi watakaoamini jambo lilo hilo? [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Amina. Wekeni mikono yenu juu hewani, na mumkubali Yesu kama Mponya wenu.

³⁸⁵ Wewe unayemwamini, hujapata kuokoka, mbona usije madhabahuni sasa hivi? Ulisema ulitaka kuwa na hisi fulani moyoni mwako kama ulivyokuwa nayo, kama aliyokuwa nayo yule mama kulungu. Unataka kumkubali Yeye kama Mwokozi wako? Utakuja hapa juu sasa na kusimama karibu na madhabahu, na uache niombe pamoja nawe wakati ukiwa katika Uwepo Wake? Wengi wenu hapa, wanapaswa kuja wasimame hapa. Kama unataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wako, njoo sasa hivi. Je! utakuja?

Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni jema.

³⁸⁶ Mtu mwingine anayetaka kumkubali? Katika Uwepo Wake, utawezaje kuwa karibu zaidi na Yeye? Kama Yeye—kama Yeye angeweza kuniambia mimi ni nini tatizo lako, ananiambia wewe unahitaji—unamhitaji Yeye. Njoo huku sasa hivi. Wewe usiye na Yeye, njoo sasa na umpokee kama Mwokozi wako binafsi. Simama hapa katika Uwepo Wake. Hata uwe nani, kama wewe ni mfuasi wa kanisa, haijalishi wewe ni nini, kama bado huko sawa na Mungu, ninakuomba, na kukusahi, katika Jina la Yesu Kristo, njoo mbele sasa kabla hatujamaliza mstari huu wa uponyaji, moja kwa moja wakati Roho Mtakatifu akiwa hapa, ambapo ninaweza kuomba maombi ya imani. Kama Yeye atanisikia mimi, kuwaponya wagonjwa, hakika atanisikia mimi kuwaokoa waliopotea. Ninyi mnaomtaka Yeye kama Mwokozi wenu, njoni mbele sasa katika Jina la Yesu. Njoni mbele sasa

na msimame karibu na madhabahu hapa kwa ajili ya maombi, kwenye wakati huu tu.

³⁸⁷ Bwana awabariki. Ninapenda hilo. Wanaume na wanawake, chini ya sadikisho, Roho Mtakatifu Mwenyewe akiwatoa moja kwa moja na kuwaleta chini madhabahuni.

³⁸⁸ Ninyi ambao mnaamini hili kuwa u—ushahidi wa ufufuo wa Yesu Kristo katika siku hizi za mwisho, kwamba, Biblia iliahidi jambo lili hili. Hilo, haiwezi ikawa ni mimi; mimi ni mwanadamu. Ni Mwokozi wenu. Ninawaambia, ni Yesu Kristo. Mkono wangu ukiwa kwenye Neno, ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kuja Kwake kumekaribia sana mpaka Yeye amejidhihirisha Mwenyewe katika utimilifu wa nguvu Zake miongoni mwa watu Wake.

³⁸⁹ Kama umekuwa na tashwishi na mvurugiko, mfuasi vuguvugu tu wa kanisa, njoo usiku wa leo ukajazwe na Roho Mtakatifu wakati Roho Mtakatifu Mwenyewe akiwa hapa, akionyesha mathibitisho yasiyokosea, kwa Maandiko, kwamba Yeye yupo hapa. Ni Yeye. Njoni sasa, kila mtu unayemtaka Yesu Kristo maishani mwako. Njoo mbele sasa na umkubali Yeye. Njoo sasa.

. . . yawezekana, amini tu.

³⁹⁰ Tunapouimba, hivi hamtakuja sasa? Loo! “Amini tu” nini? Amini tu Ukweli wa Biblia, yale ambayo mmeambiwa. Yeye Huyu hapa, akilithibitisha. Kwa nini Yeye akaniambia, moja kwa moja katikati ya ibada hiyo ya uponyaji? Kwa nini aliniambia katika ibada hiyo ya uponyaji, “Waite watu madhabahuni”? Huenda ikawa ni nafasi ya mwisho ya mtu fulani. Sijui mimi. Jambo pekee nijualo, ni, kumtii Roho.

. . . amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

Bwana, naamini, Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana,

³⁹¹ Vema, ndugu wahudumu, papa hapa chini, moja kwa moja chini upande huu.

. . . amini . . .

Nafasi hiyo moja, ndugu. Nendeni chini kabisa. Hebu watenda kazi wa binafsi wakusanyiike hapa sasa. Tunaenda kuomba kwa ajili ya watu hawa.

. . . Naamini; Ee Bwana, naamini;
Mambo yote yawezekana,

³⁹² “Hivi inawezekana mimi kumpokea Roho Mtakatifu kama walivyofanya katika Siku ya Pentekote?” Hakika, kama ukiamini.

. . . amini.

Amini tu,

³⁹³ Je! unataka tukio halisi la upendo wa Mungu, kama yule mama kulungu alivyokuwa nao kwa ajili ya mtoto wake? Ikiwa ujuzi wako hauko hivyo, umepungukiwa. Njoo huku. Kama unataka kumdhihirisha Yesu Kristo maishani mwako, njoo huku. Usiigize kanisa tena.

³⁹⁴ Saa imewadia, haitupasi kukichezea kitu hiki kikuu ambacho Mungu ametupa, mathibitisho yasiyokosea ya Yesu Kristo akiwa hai leo baada ya miaka elfu mbili iliyopita. Hivi hutakuja? Kanisa linapokea karama yake ya mwisho. Hili ndilo jambo la mwisho litakalolijia Kanisa kabla ya Kuja kwa Kristo, kulingana na Neno la Mungu. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Mwana wa Mungu.” Sisi hapa.

³⁹⁵ Njoo, sivyo, kila nafsi isiyomjua Yeye, kila nafsi iliyo na shaka usiku wa leo? Usiache nafasi hii nzuri sana ikupite. Mbona usije sasa na kusimama kwa ajili ya maombi wakati tunapokusanyika mahali hapa? Hiyo ni kweli. Endeleeni tu kuja. Sisi, tunataka kuwaona, kila mtu ambaye ni... Tunangojea kidogo tu, kwa sababu kweli ninajisikia wapo wengine hapa wanaopaswa kuja, haijalishi umejishirikisha na kanisa gani. Hatukuulizi kwa ajili ya ushirika wa kanisa. Tunakuomba uje, umpokee Kristo. Hivi ungetaka kumpokea yule Mungu ajuaye siri za moyo, anayeweza kuzifunua papa hapa kama alivyofanya, anayejua mawazo yenyewe unayowazia, na anaweza kuyaelezea kwako, kama Yeye alivyofanya katika siku zilizopita? Sasa, Bwana abariki.

³⁹⁶ Sasa, wakati hawa wameyazunguka madhabahu, na wakati wengine wanapokuja, hebu walio katika kusanyiko wasimame kwa dakika moja tu sasa, wakati tunapoenda kuomba. Sasa, nyinyi mlio wagonjwa huko nje ambao labda hamkuwa kwenye mstari wa maombi, wekeaneni mikono mmoja kwa mwingine. Hebu watenda kazi wote wa kibinafsi na wahudumu waweke mikono juu ya watu hawa hapa.

³⁹⁷ Mko tayari? Mmeona kitu ambacho ni halisi? Kitu fulani kimeuchochea moyo wako? Kitu fulani kimekuwa halisi kwako, upesi, kujua ya kwamba Yesu Kristo yu hai usiku wa leo?

³⁹⁸ Sasa hebu tuviinamishe vichwa vyetu, na kila mtu aombe kwa njia yako mwenyewe. Kumbukeni, kuna mamilionni ya maombi yanayopaa juu kote ulimwenguni sasa hivi. Mungu husikia kila moja wao, kwa sababu Yeye hana kikomo. Omba sasa kama unavyofanya katika kanisa lako mwenyewe. Mwombe Mungu akusamehe dhambi zako. Omba ili Yeye akujaze na Roho Mtakatifu. Omba ili Mungu akuponye. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu na ashuke namna hiyo miongoni mwenu na awape ushindi mkubwa na uhuru.

³⁹⁹ Baba wa Mbinguni, tunawaleta wasikilizaji hawa Kwako sasa hivi. Jalia nguvu kuu zilizomfufua Yesu Kristo kutoka kaburini, jalia zilihuishe kanisa hili sasa hivi. Naomba uponyaji uje. . . Jalia kila mtu aliye mgonjwa akombolewe kutokana na nguvu za Shetani. Jalia kila nafsi iliyopotea iokolewe, na kila mtu aliyeokoka ajazwe na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

⁴⁰⁰ Omba kama vile hujawahi kuomba hapo kabla. Omba kana kwamba ulikuwa unakufa, kana kwamba ni dakika yako ya mwisho, na Mungu atalijalia. 

63-0605 Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa
Ramada Inn
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org